UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA WADAU BINAFSI WA MISITU KIBIASHARA KUHUSU RASIMU YA SERA PENDEKEZI YA MISITU

Maoni ya kuchangia kwenye mchakato wa mapitio ya sera ya misitu yaliyowasilishwa na wadau wa sekta binafsi ya kupanda miti kibiashara wa nyanda za juu kusini

28 Agosti 2017

Makala ya mwisho baada ya warsha ya kuchambua sera pendekezi iliyofanyika tarehe 18 Agosti 2017

Taarifa hii ya usanisi yenye lengo la kuboresha shughuli za upandaji miti nchini Tanzania zimejikita katika maoni na taarifa zilizotolewa na wadau binafsi wa upandaji miti kibiashara wa Nyanda za juu Kusini. Ni taarifa iliyoandaliwa baada ya mfululizo wa mikutano kadhaa ya mashauriano iliyofanyika kati ya mIezi ya Julai na Agosti mwaka huu na kuhudhuriwa na wafanya biashara wadogo na wa kati, vyama vya ushirika kama vile UWAMBA, SAFIA, NOFIA na SHIVIMITA, wafanya biashara wa nguzo za miti,wenye mashamba makubwa ya miti na wenye viwanda vya kuchakata magogo ya mbao, Watoa huduma za kustawisha miti, wafanyabiashara wa mbao na wasafirishajipamoja na wauzaji wa nguzo ambazo hazijatiwa dawa.Washiriki wa warsha walipitia rasimu ya Sera ya Taifa ya Misitu wa mwezi Oktoba 2016 (URT,2016). Waliowezesha warsha hiyo kufanyika ni Taasisi ya Uendelezaji Misitu Tanzania (FDT).

MUHTASARI

Idara ya Misitu na Nyuki chini ya Wizara ya Mali Asili na Utalii iko katika mchakato wa kupitia upya Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 kwa kushauriana na wadau mbalimbali nchini.

Upandaji miti kibiashara ni mojawapo ya shughuli za kiuchumi zinazo liingizia taifa mapato, ajira, na upatikanaji wa malighafi na mazao ya timbao kwa ajili ya viwanda vingi. Hata hivyo upo uwezekano mkubwa wa sekta ya misitu kuweza kuchangia zaidi ikilinganishwa na baadhi ya nchi duniani kwa mfano Uruguay, endapo Sera ya Taifa Misitu itafanyiwa marekebisho madogo kuhusu uwekezaji.

Warsha ihusuyo usanisi na kuhalalisha / kuthibitisha sera ya misitu ilifanyika 18 Agosti kuwezesha wadau kutoka sehemu mbalimbali na wenye uzoefu wa kila aina kutoa maoni yao na kutoa muhitasari wa mawazo yote waliyoyaona yangefaa kuongezwa kwa nia ya kuiboresha rasimu. Mapendekezo yalipatikana kwa wao kukaa katika vikundi wakati wa warsha na mapendekezo yao waliyatuma kwa Timu ya Kitaifa ya kupitia na kuchambua sera mpya pendekezi ya misitu.

Katika mwezi wa Julai na Agosti, 2017 wadau binafsi wa panda miti kibiashara wa Nyanda za juu Kusini, walikutana kujadili mswaada- jaribio wa sera ya misitu na kutoa mapendekezo yao / maoni yao namna ya kuiboresha kulingana na mahitaji yao.

Hivyo waraka huu ni muhtasari wa yote yaliyochambuliwa na kupendekezwa. Taasisi ya Uendelezaji wa Misitu Tanzania (FDT) ndiyo waliofadhili uendeshaji wa warsha/kongamano hilo. Upeo wa waraka huu unagusa tu maoni yaliyotolewa na wadau wa Nyanda za juu Kusini ambao walijikita katika mazao ya timbao yatokanayo na mashamba makubwa ya miti. Waliohudhuria warsha hiyo ni pamoja na wakulima wa miti wa viwango mbalimbali, wachakataji wa mazao ya misitu, makampuni, na watoa huduma za misitu.

Mapendekezo yao, yahusuyo upandaji miti kibiashara ambayo yaliyotokana na warsha ya kusanisi na kuhalalisha / kuthibitisha rasimu ya Sera mpya ya taifa ya Misitu ni pamoja na:

WASHIRIKA BINAFSI WA PANDA MITI KIBIASHARA WATAMBULIWE KATIKA SERA YA MISITU

Sekta ya panda miti kibishara imekuwa ikichangia sana kutimiza malengo ya serikali ya kiuchumi, kijamii na ya hifadhi ya mazingira, hata hivyo panda miti kibiashara imekuwa sekta ambayo haijatambuliwa au kukuzwa vilivyo na serikali. Washikadau wanapendekeza kuwa kuna umuhimu wa Sera ya Taifa ya Misitu kutambua na kuiunga mkono sekta binafsi ya panda miti kibiashara katika majukukumu yake ya shughuli za kiuchumi, kijamii, na uhifadhi wa mazingira nchini Tanzania.

MASWALA YA KISERA KUHUSIANA NA UENDELEZAJI WA MASHAMBA MAKUBWA YA MITI

Mapendezo ya washidau yalijikita zaidi katika maswala yanayohusu ardhi ya kupanda miti, shughuli za ugani, na huduma mbalimbali, moto, wadudu waharibifu na magonjwa ya miti.Kwa kuwa inafahamika kuwepo kwa uhaba wa ardhi kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya miti, na kuwa serikali inayo ardhi wazi inayomilikiwa na TFS, serikali za mitaa (LGAs) na wananchi, wadau wako makini katika kushirikiana na serikali kuhakikisha ardhi hiyo inatumika kwa uangalifu mkubwa, kupitia mpango wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali (PPP). Isitoshe moto kichaa unazidi kuwa tatizo kuu, linaloathiri mashamba makubwa ya miti nchini.

Hivyo wadau wanashauri serikali kuunda taasisi maalum ya kitaifa kwa lengo la kuchunguza matukio ya moto, kutambua, kuzuia na kuzima moto unapotokea. Ili kudhibiti mlipuko wa wadudu waharibifu na

magonjwa, serikali imeshauriwa kuanzisha kitengo cha kufuatilia matukio hayo chenye uwezo mkubwa wa utoaji taarifa sahihi juu ya matukio hayo. Mapendekezo mengine yaliihusu serikali kuwasaidia wazalishashaji wa mbegu za miti ili waweze kuzalisha mbegu zenye ubora wa hali ya juu hapa hapa nchini ili nchi iweze kujitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora za miti.

Yalitolewa malalamiko kuwa, shughuli za ugani wa misitu nchini zilikuwa hafifu mno kana kwamba hawakuwepo wagani wa misitu nchini. Hivyo serikali ifufue upya shughuli za ugani kwa kuziimarisha na kuwapa madaraka vyama vya wapanda miti (TGA) kutoa huduma za ugani wa misitu siku za usoni.

MASWALA YA KISERA KUHUSIANA NA UENDELEZAJI WA VIWANDA VYA MISITU

Kilio kikubwa cha wadau kilikuwa ukosefu mkubwa wa malighafi za timbao, mitaji, tekinologia ya kale, upungufu wa watalaam, na mazingira yasiyo rafiki ya kibiashara. Kutokana na hali hiyo, wadau walishauri serikali kuendelea kufanya tathimini ya wingi na ubora wa mali ghafi za timbao kwa ajili ya viwanda, malighafi ambayo inapatikana katika mashamba makubwa ya miti ya watu binafsi na ya serikali, ili kutumia taarifa hizo kwa ajili ya kulinganisha mara kwa mara mahitaji halisi ya malighafi ya mazao ya timbao na rasilimali ya misitu iliyopo kitaifa.Yalitolewa pia mapendekezo kwa serikali kutoa ruzuku kwa vifaa na mitambo inayoagizwa kutoka nje kwa ajili kuchakata mazao ya timbao na kuyaongezea thamani mabaki yake. Vile vile serikali ilishauriwa kuboresha utaratibu wa kuandaa kanuni za viwango vya mazao ya timbao kukidhi ubora wa kimataifa na wa hapa nchini. Hatimaye ushauri wa kurekebisha na kuongeza mitaala mipya katika vyuo vya misitu kwa nia ya kuondoa udhaifu wa utendaji kazi katika sekta ya misitu ulisistizwa.

JINSI YA KUINUA SHUGHULI ZA PANDA MITI KIBIASHARA NCHINI

Sekta binafsi ya misitu nchini Tanzania inajiendesha bila utaratibu mzuri na usio kuwa na utawala thabiti kuiwezesha sekta hiyo kupeleka maoni yake serikalini.

Jambo la pili ni kuwa sekta yenyewe bado ni changa sana na yahitaji kutunzwa ili iwe imara na yenye mfumo mzuri kuiwezesha kuchangia kiuchumi kadri inavyostahili. Serikali ilishauriwa kuwa na utaratibu wa kuiwezesha sekta binafsi ya misitu kupata wawakilishi wanaotokana na vyama vyao vya kisheria kwa madhumuni ya kuwa na jukwaa la majadiliano na mashauriano na serikali. Mapendekezo mengine ya kisera mtambuka ni, ya serikali kujenga mazingira mazuri na yenye motisha ya kuanzisha ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali katika nyanja za uzalishaji, uchakataji, ongezeko la thamani, masoko ya mazao timbao na yasiyo ya timbao. Zaidi ya hayo inatakiwa serikali itoe ruzuku na misaada ya fedha, kuiwezesha sekta binafsi ya misitu kutekeleza shughuli zake kutokana na mchango wake mkubwa kiuchumi.

Kwa kuongezea tu ni kwamba barabara karibu zote mahali ambapo shughuli za upandaji miti kibiashara hufanyika, imeonekana kuwa miundo mbinu ya barabara hizo hairidhishi na wakati mwingine huwa katika hali mbaya kabisa. Serikali inashauriwa kuzikarabati na kuzitengeneza barabara hizo mara kwa mara, kwa nia ya kuboresha miundo mbinu katika maeneo hayo. Msisitizo juu ya utafiti ulionekana wazi wazi kwa washikadau, na serikali ilishauriwa kutenga fedha ya kutosha kuziwezesha taasisi za utafiti kuimarisha uwezo wao wa utafiti wa misitu.

1. DIBAJI

Idara ya Misitu na Nyuki ya Wizara ya Mali Asili na Utalii iko katika mchakato wa kupitia upya Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998. Rasimu ya kwanza wa sera ya Taifa ya Misitu ulitolewa mwaka 2004 na kufuatiwa na mapitio mengine miaka ya 2010 na 2016. Kazi hiyo imekuwa ikifanyika kwa ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na hivyo kuanzishwa kikosi kazi, mashauriano na wadau mbalimbali ambao kwa pamoja waliweza kuandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Misitu uliochapishwa mwaka 2016 (FBD, 2017) Shughuli hii ya kukusanya maoni itazingatia agenda mbalimbali zikiwemo: misitu ya hifadhi, utunzaji wa misitu ya kijamii, mabadiliko ya tabia nchi, na upandaji miti kibiashara. Katika utekelezaji wa kazi hii, mikutano ya kanda imekuwa ikifanyika nchi nzima.

Upandaji miti kibiashara ni shughuli kubwa ya kiuchumi nchini (kwa mfano zaidi ya kaya 60,000 hustawisha miti katika Nyanda za juu Kusini), na ni mojawapo ya sekta inayoliingizia taifa mapato makubwa, huku sekta ikiajiri watu wengi, na ni chanzo cha malighafi ya mazao ya timbao yanayohitajika viwandani. Sekta binafsi imechangia pakubwa katika kuikuza sekta ya panda miti kibiashara kwa kuwainua wakulima wa mashamba ya miti, kukuza biashara za mbao, makampuni, na watoaji wa huduma za misitu.

Katika miezi ya Julai na Agosti, 2017 wadau wa panda miti kibiashara wa Nyanda za Juu Kusini walikutana ili kuipitia upya rasimu ya Sera ya Taifa ya Misitu. Waraka huu ni muhtasari wa maoni na mapendekezo yao. Mapendekezo na maoni haya yatawasilishwa kwenye kikosi kazi cha Wizara ambacho kitahitimisha mchakato wa uandaaji wa muswada wa mwisho wa Sera ya Taifa ya Misitu.

Mapendekezo na mawazo yaliyotolewa kutokana na uzoefu wa wadau wa Nyanda za juu Kusini yamejikita zaidi katika mazao ya timbao yanayotokana na mashamba ya miti na si vinginevyo.

Taasisi ya Uendelezaji wa Misitu Tanzania (FDT) ilichangia kuwezesha mchakato huu wa kupitia upya sera ya misitu. FDT ni Taasisi ambayo imeanza kufanya kazi zake nchini kuanzia mwaka 2013 na imejianzishia mahusiano mazuri na wadau wa upandaji miti kibiashara na kujipatia uzoefu mwingi wa namna ya kuwawezesha wadau waweze kukuza na kuboresha shughuli zao za upandaji miti kibiashara. Orodha nzima ya walioshiriki kwenye mchakato huo imeonyeshwa katika kiambatisho (1).

Mapendekezo ya washikadau yamegawanyika katika sehemu kuu nne, husan: sera zenye kipaumbele zaidi zikiwa ni pamoja na kutambuliwa kwa sekta binafsi ya upandajipanda miti kibiashara, mashamba makubwa ya miti, viwanda vya uchakataji wa mazao ya timbao, na uwezeshaji wa sekta nzima ya upandaji miti kibiashara. Kila kipengele kilichotajwa kimeandaliwa kwa kuzingatia:

1. Mtazamo wa jumla sera ilivyo kwa muonekano wa wadau binafsi;
2. Taarifa muhimu zinazopatikana nchini, zikiwemo za sekta binafsi, na za miradi ya maendeleo ya misitu inayofadhiliwa na FDT na PFPT;
3. Uzoefu wa nchi nyinginezo za Kiafrika (zikiwemo Ghana, Kenya, Nigeria, Afrika ya Kusini, Uganda, Zambia na Zimbabwe) na nje ya Afrika hususan Uruguay; na
4. Mapendekezo mengineyo yaliyopelekwa kwenye timu ya kupitia sera ya misitu upya (ikizingatiwa kuwa baadhi ya mapendekezo haya yatashughulikuwa na sekta nyingine za serikali zenye mafungamano makubwa na sekta ya misitu (k.m Ardhi, Hazina, na Miundo mbinu).

Angalizo: Taasisi ya Uendelezaji wa Misitu Tanzania (FDT) haiwajibiki kwa Mapendezo na mawazo yote ya makala haya-

2. MAPENDEKEZO YA KISERA

2.1 WAPANDA MITI KIBIASHARA NA WASHIRIKA BINAFSI WA SEKTA YA MISITU WATAMBULIWE KATIKA SERA YA MISITU

Maoni ya wadau

Upandaji miti kibiashara una mchango mkubwa katika uchumi wa nchi kwa kutengeneza ajira vijijini, kuongeza kipato, uzalishaji wa malighafi ya viwanda na faida nyingne nyingi zisizoeleweka kwa urahisi k.m. hifadhi ya udongo na maji, kurejesha misitu iliyotoweka, na kurekebisha hali ya hewa. Upandaji miti kibiashara pia unasaidia kupunguza uharibifu wa misitu ya asili kwa kutoa mazao ya mitimbao ya kutumiwa humu nchini na kuuza nchi za nje badala ya mazao hayo kuvunwa kwenye misitu ya asili pekee.

Kwa ujumla pamoja na kwamba upandaji miti kibiashara una mchango mkubwa sana kijamii na kiuchumi, hata hivyo hakuna jitihada za kuiendeleza na kuikuza ipasavyo sekta hiyo. Na haijatambulika rasmi katika Sera ya Taifa ya Misitu. Misitu ya jamii na misitu ya kibiashara yote imewekwa katika kifungu kimoja cha sera ya misitu, wakati kwa hakika misitu hiyo hutofautiana katika majukumu na mahitaji yao. Hivyo kisera, shughuli hizo zinapaswa kuwekwa kwenye vifungu vinavyojitegemea. Wadau wanafikiria **kuwa Sera ya Taifa ya Misitu inatakiwa kutambua na kukuza kwa ukamilifu dhima ya upandaji miti kibiashara na wadau binafsi katika kuunga mkono malengo yake ya kuinua uchumi, hifadhi ya mazingira na maendeleo ya kijamii nchini. Sera yapaswa kuwa na mkakati wa namna ambavyo sekta binafsi itawezeshwa na kuendelezwa.**

Hali ilivyo Tanzania

Sekta binafsi ndiyo inayoongoza kwa kumiliki mashamba makubwa ya miti, na ndiyo yenye kasi kubwa ya upanuzi wa mashamba mapya na maeneo mapya. Mwaka 2011, Indufor ilikadiria kuwa hekta zinazomilkiwa na vijiji na watu binafsi ni kati ya 80,000 hadi 140,000. Mwaka 2016 FDT nao kwa kutumia satellite na data nyingine walikadiria kati ya hekta 160,000 na 175,000 zinazomilikiwa na wakulima wadogo na wa kati. Upandaji miti ni shughuli kubwa, FDT ikikadiria shughuli hiyo kufanywa na wakulima wapatao 60,000 wa Nyanda za juu Kusini FDT (2016). Mengi ya mashamba hayo yanastawishwa kwenye ardhi binafsi au kwa ubia na serikali. Mashamba ya wakulima wadogo na wa kati ni aslimia 68% ya mashamba yote ya nyanda za juu Kusini (hekta 233,000 hadi 257,000), huashiria jinsi mashamba makubwa ya miti ya umma na ya binafsi yalivyochukua sehemu ndogo tu ya ardhi nchini. Kwa kupima uchumi na kasi ya ongezeko la watu inakisiwa kuwa mahitaji ya mazao ya misitu yatazidi matumizi kwa zaidi ya mita za ujazo 2.2 millioni ifikapo mwaka 2030. Hii ni sawa na upungufu wa hekta 7,000 hadi 8,000 za miti iliyopandwa, kwa makisio ya uvunaji wa mita za ujazo 300 hadi 400 kwa hekta moja.

Viwanda vya misitu huchangia upatikanaji wa mapato serikalini kutokana na kodi. Mwaka 2013 na 2014 TFS walikusanya kodi ya mapato kiasi cha Sh. 1.53 billioni. Halmashauri za wilaya zilikusanya Sh. 2,2 billioni na VAT Sh. 17.99 billioni. Vile vile sekta binafsi inaongoza kwa umiliki wa sekta ya viwanda vya misitu, sekta ambayo imeibuka upya. Viwanda hivyo huzalisha bidha zilizoongezewa mnyororo wa thamani katika mashine za kuchakata mbao, viwanda vya plywood, karatasi, nguzo, samani, na viunganishi. Kumeibuka kwa kasi utengezaji wa venia kwa kutumia magogo madogo ya mikaratusi. Viwanda vya misitu huajiri takribani asilimia 80 % ya wafanyakazi vijijini wanaotumika katika uzalishaji huo wa mnyororo wa thamani, ambao kwa mwaka hutengeza ajira za watu wanaofikia 20,000 hadi 30,000 kwa mwaka (PFP, 2016).

Changamoto za viwanda vyote vya misitu nchini zinafanana, ikiwa ni pamoja na uchakavu wa mitambo, tekinologia iliyopitwa na wakati, ufanisi wa chini katika kuchakata na kuvuna mazao ya timbao, utalaam mdogo wa kusimamia na kuendesha viwanda, ugumu wa upatikanaji wa fedha za uwekezaji na mkakati wa kutafuta masoko (Indufor, 2011; PFP, 2014). Pamoja na changamoto hizo, viwanda vya misitu ndio vimechangia fedha nyingi, karibu nusu ya mapato yote ya mchango wa sekta ya misitu kwenye pato la taifa/GDP (MNRT 1998; NFP 2001-2010). Mchango huu pekee ungetosheleza kwa serikali kuitambua sekta hii na kutoa motisha za kifedha za uwekezaji kibiashara kwenye viwanda vya misitu. Hitaji hili ni muhimu ukizingatia hasa nyaraka za serikali kuhusu maendeleo ambazo ni pamoja na:

- Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Viwanda ya mwaka (1996 - 2020), inayosistiza kukuza viwanda vidogo na vya kati kwa kutumia kila aina ya mbinu.
- Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 (FYDP II), wenye kauli mbiu ya kutunza viwanda ili kubadilisha uchumi na maendeleo ya watu kuwa bora zaidi".
- Mkakati wa maendeleo ya viwanda vinavyotegemeana (2025), ikiwa ni mwendelezo wa Mpango wa Taifa wa miaka mitano (ii) kwa kulea mabadiliko ya biashara zilizo katika hatua ndogo ziingie hatua ya kati hadi hatua ya biashara kubwa pamoja na uongezaji wa mkusanyiko wa viwanda, ngazi ya vijiji na Wilaya.
- Sera ya Taifa ya kukuza uchumi wa mwananchi (2004), Inayozitaka sekta zote za Wizara kuandaa mazingira mazuri ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza uchumi.

Mapendekezo:

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika sera mpya:

● Iongezwe fasili ya wazi kutofautisha sekta ya panda miti kibiashara kama sekta ya aina yake inajumuisha viwanda vya misitu na wakulima wa miti, na umiliki wa misitu utofautishe kati ya misitu inayomilikiwa na jamii na ilnayomilkiwa kibiashara.

● Serikali iandae mwongozo wa kutoa motisha na uungawaji mkono katika kuendeleza sekta binafsi ya kupanda miti kibiashara.

● Kwa kutambua mchango mkubwa wa kiuchumi unaotolewa na sekta ya panda miti kibiashara, Idara ya Misitu iwe na kitengo ama dawati la kushughulikia sekta ya panda miti kibiashara.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Uganda inatoa mfano dhahiri wa sera ya wazi kutambua sekta ya mashamba ya miti kibiashara.

Kisanduku Na 1. Sera ya Taifa ya **Uganda** inayotambua wadau wa aina tofauti na inayounga mkono mashamba makubwa ya miti"Serikali ya Ugandainatambua aina nyingi za watu wenye kuguswa na sekta ya misitu, watu ambao mahitaji yao ya misitu hayajatafutiwa ufumbuzi kikamilifu, na ambao wajibu wao unatakiwa kufafanuliwa / kufasiliwa na kuratibiwa kwenye utekelezaji wa sera. Wengi wa waliotambulika katika sera ni pamoja na: wazalishaji wa mazao ya misitu (wakulima, wakuzaji miti kitiashara, na wamilki wa mashamba ya miti), watumiaji wa mazao ya misitu (watumiaji miti kibiashara, na wengi wa waishio mijini na masikini wa vijijini wanaotegemea kuni na mazao mengine ya misitu kujikimu).

Wachakataji wa mazao ya misitu (wachoma mkaa, wapasua mbao, mafundi mchundo, na wafanyabiashara) na jamii yoyote inayoguswa na shughuli za misitu; mashirika ya kiserikaly na yasiyo ya kiserikali, na watu ambao hutoa huduma za usimamizi, mafunzo, utafiti na usaidizi.". Biashara za mashamba ya miti zenye tija zitakuzwa., Sekta binafsi itapewa nafasi kubwa kuendeleza na kutunza mashamba ya miti ya kibiashara. Hilo litafanyika kupitia mashamba makubwa ya misitu kwenye ardhi ya serikali ama ardhi binafsi, au kwenye mashamba madogo ya miti. Kazi ya erikali itakuwa kusimamia na kudhibiti maendeleo hayo.

Mfano wa **Uruguay** unadhihirisha jinsi ambavyo ubadilishaji sera yalivyoleta mabadiliko katika sekta ya misitu. Na hii ni muhimu ikizingatiwa sekta ndogo ya panda miti kibiashara inayo nguvu kubwa nchini Tanzania.

Sanduku na 2. Mabadiliko ya sekta kutokana na mabadiliko ya Sera- Mfano wa sekta ya misitu ya **Uruguay** katika miaka ya 1980, matumizi ya mazao ya misitu yaliyofikia tani million 2 kwa mwaka yaliyozidi uzalishaji kwa mwaka wa tani million 1.3, hali iliyosababisha uvunaji mkubwa wa misitu ya asili, kuiacha Uruguay kuagiza mazao ya misitu kutoka nje ya nchi. Mwaka 1987, Uruguay ilibadilisha sharia ya misitu, hali iliyobadilisha mambo. Mwaka 2013, Uruguay ilijipatia dola za kimarekani 70 millioni ikiuza mazao ya misitu nchi za nje yenye kufikia aslimia 6% ya mauzo yote ya nje. Kiasi cha misitu kiliongezeka mara mbili na kufikia asilimia 10% mwaka 2010, huku misitu ya asili ikiongezeka kwa asili 6.5 kutoka hekta 719,000 mwaka 1990 hadi hekta 766,000 mwaka 2010, huku mashamba ya miti yakiongezeka mara 30 kutoka hekta 31,000 miaka ya 1980 na kufikia hekta 978,000 mwaka 2010. Ajira imeongezeka mara tano tangu mwaka 1989. Mafanikio ya sheria mpya ilichangiwa na kung'amua changamoto kuu zilizokuwa zikiikumba sekta ya upandaji miti kibiasharana utafutaji wa mbinu za kushinda changamoto hizo. Ufumbuzi wa matatizo hayo ilikuwa ni kutenga hekta million 3.6 za ardhi inayofaa kwa usitawishaji wa mashamba makubwa ya miti kwenye kanda zinazofaa, misamaha ya kodi za ndani, misamaha ya ushuru wa uingizaji wa bidhaa za uzalishaji na bidhaa za kukuza mitaji, serikali kuwekeza kwenye miundombinu ili kuwezesha usafirishaji wa mazao ya misitu kwenda sokoni, ruzuku hadi kufikia asilimia 20-50 za kufidia gharama za upandaji miti, na mikopo nafuu ya kuwekeza katika uanzishaji wa mashamba ya miti, uvunaji wa magogo, na utengenezaji wa bidhaa za misitu kwa nia ya kuongeza thamani. Mafanikio ya sera yaliifanya Uruguay kuondoa ruzuku mwaka 2005, bila kuathiri uwekezaji zaidi. Kwa sasa Uruguay ni miongoni mwa nchi zenye sekta ya misitu ya hali ya juu iliyosheheni makampuni ya ndani naya kigeni yanayozalisha mazao mengi ya misitu kwa matumizi ya ndani na uuzaji nchi za nje.

Sanduku la 3. Kutofautisha na kufasili misitu ya jamii na misitu binafsi ya upandaji miti kibiashara---**Kenya, Uganda** na **Nigeria.** Sera ya Taifa ya misitu ya Kenya inafasili Misitu ya jamii kama" ardhi ya misitu ambayo kisheria inamilikiwa, kutunzwa au kutumiwa na aina fulani ya jamii," wakati Misitu binafsi inahusisha "ardhi ya misitu inayomilikiwa na mtu yeyote kihalali au ardhi ya kukodi na msitu wowote unaomilikiwa na mtu binafsi, taasisi, au chombo chochote cha kibiashara au kisicho cha kibiashara kinchatambuliwa kipekee". Vivyo hivyo nchi za Uganda na Nigeria zinachulia misitu ya aina hiyo kwa kuitofautisha.

2.2 MASUALA YA KISERA KUHUSIANA NA UENDELEZAJI WA MASHAMBA MAKUBWA YA MITI

2.2.1 UPATIKANAJI NA UMILIKI WA ARDHI

Mawazo ya wadau

Upungufu wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya misitu ni changamoto kubwa katika uendeshaji wa viwanda ambavyo vingi vyao huendeshwa chini ya asilimia 40-50% tu ya uwezo wake. Upungufu huo unatarajiwa kuongezeka, na kuna hatari ya uzalishaji wa malighafi kutoka vyanzo vya ndani kutotosheleza mahitaji ya viwanda vya ndani. Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya miti umekuwa na changamoto kubwa kwa sababu ya mlolongo mrefu wa kisheria na kiutawala unaohitajika kufuatwa kabla ya kupata ardhi. Kutokana na upungufu wa ardhi kwa upandaji wa miti na huku ikizingatiwa kwamba serikali inamiliki maeneo ya ardhi chini ya Mamlaka ya huduma za Misitu ambayo yangefaa kwa upandaji miti, wadau wako tayari kushirikiana na serikali kuhakikishaa kuwa ardhi iliyowazi inatumiwa ipasavyo. Wadau wanafikiria kuwa Sera ya Taifa ya Misitu iwe mstari wa mbele kuendeleza uanzishwaji wa mashamba makubwa ya miti na kusimamia ufanisi wa uendeshaji wa mali asili za misistu zilizopo, pamoja na kutoa baadhi ya ardhi ilyyotengwa kwa ajili ya mashamba ya misitu ya serikali kutumiwa na sekta binafsi kuendeleza misitu kwa njia ya makubaliano, au kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (Public Private Parnterships/PPP).

Hali ilivyo Tanzania

Ngaga (2011) aliandika kuwa serikali inamilki kiasi cha hekta 72,000 ambazo baadhi yake hazijaendelezwa, na wakati huo huo wawekezaji binafsi hawana ardhi ya kutosheleza mahitaji yao, na umilikishaji wa ardhi katika baadhi ya sehemu nchini haueleweki vilivyo. Tatizo hili limezidishwa na wilaya na vijiji kutokuwa na mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi. Mpango wa matumizi bora ya ardhi ni muhimu sana katika kutambua maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa upandaji miti kibiashara. PFP (2016) nao wamesisitiza kuwa mpango mzuri wa matumizi bora ya ardhi ufanyike ili kuzuia fursa za uwekezaji kupotea.

Nchini Tanzania, mipango ya Ubia kati ya Sekta ya Uma na Sekta Binafsi (Public Private Parnerships/ PPP) inaendana kwa pamoja na Sera ya Taifa ya Ubia kati ya Sekta ya Binafsi na Sekta ya Uma ama Public Private Partnership (2009), lakini inabidi itafsiriwe namna ambayo misitu itakuwa sehemu ya ushirikiano huo. Namna nyingine za ushirikiano zinazoweza kutumika ni sekta binafsi kwa sekta binafsi, sekta binafsi na Jamii, au wa sekta za sekta ya uma kwa sekta ya uma. Rasimu ya sera ya taifa ya uwekezaji ya huduma za misitu/Tanzania Forest Service Investment Policy (2015), " unataja kuwa mahali ambapo kuna upungufu wa rasilimali chini ya Wakala wa misitu ambazo zinastahili kutumika kwa uwekezaji, TFS yapaswa kushirikisha sekta binfsi zenye uwezo kupitia PPP, kama ilivyopendekezwa katika sera ya uwekezaji. Sera pia insisistiza kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi. PFP (2015) ilisisitwa kuwa kanuni, sharia, taratibu na miongozo ya makubaliano ya kukata miti kwenye misitu ya serikali ya akiba na mashamba makubwa ya miti zirekebishwe na kufasiliwa vizuri.

Mapendekezo

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya taifa ya misitu:

● Serikali itafanya marekebisho ya taratibu za umiliki wa ardhi wa ajili ya shughuli za misitu na matumizi menginge na kuurahisisha na kuufanya uwe na tija kuliko ilivyo sasa, ili kuhamasisha uwekezaji. Mipango ya matumizi bora utatiliwa mkazo kuviwezesha vijiji kutenga maeneo ya ardhi kwa matumizi mbalimbali yakiwemo ya upandaji wa miti. Sheria za umiliki wa ardhi zitazingatiwa kwa nidhamu ya hali ya juu kuepuka ubadhirifu na utapeli.

● Kwa shabaha ya kuongeza ukubwa wa mashamba ya kupanda miti kibiashara serikali itatekeleza mpango wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (public private partnerships/PPP) kwa (a) kukodisha misitu ya hifadhi ya serikali kwa kuwekeana mikataba ya kumiliki ardhi (b) kutenga maeneo ya misitu yaliyoathirika kimazingira kwa mikataba ya PPP inayozingatia matakwa ya pande zote mbili.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na 4: Sera ya Taifa ya Misitu ya **Uganda** inayounga mkono uanzishwaji wa mashamba makubwa ya miti.

" Serikali itandaa mazingira mazuri kwa wawekezaji katika mashamba makubwa ya miti. Serikali pia itatenga ardhi inayofaa kwa ustawishaji wa miti kwa ajili ya nishati, magogo, na misitu ya kuhifadhi hewa ukaa katika maeneo mbalimbali ya nchi pia kuweka kipaumbele cha kupanda miti kwa ajili ya kuni kwenye maeneo ya kuzunguka miji.

Mkakati wa utekelezaji wa sera hii ni pamoja na:

Kuimarisha mikataba ya kisheria kati ya serikali na wawekezaji binafsi kwa ajili ya matumizi ya hifadhi za misitu, na kupitia kanuni za sheria ya misitu na umiliki wa ardhi kwa madhumuni ya kuhamasisha maendeleo ya upandaji miti kibiashara.

Kupitia upya sheria za uwekezaji nchini kuwezesha uanzishwaji wa mashamba makubwa ya viwanda vya misitu. Hatua kwa hatua usimamizi wa mashamba makubwa ya miti yaliyo kwenye hifadhi za misitu uhamishiwe kwenda kwenye sekta binafsi.

Kwa kuongezea, sera iwe na kipengele cha *"kuruhusu uvunaji wa mashamba ya miti ya serikali kwa njia ya kuendesha mnada kiushindani kwa shabaha ya kuongeza ukweli na uwazi, kuongeza mapato ya serikali na kuonyesha kwa uwazi kabisa thamani ya rasilimali zilizopo katika misitu ya serikali."*

Mamlaka ya taifa ya misitu ya Uganda imehamasisha sekta binafsi kustawisha hekta 60,000 za mashamba bora ya miti kwenye ardhi ya umma katika kipindi cha miaka 10. Zoezi hilo hufanyika kwa kuzingatia sifa anazostahili kuwa nazo mwekezaji, umiliki wa ardhi, miaka ya kumiliki ardhi, gharama na kanuni za usimamizi wa mashamba ya miti. Ushauri hutolewa kwa wakulima wa miti na kupima maendeleo yao ya kilimo cha miti kwa ukaribu sana kama njia mojawapo ya mpango wa utoaji wa motisha kwa wakulima hao. Sekta binafsi ya Uganda ni mchanganyiko wa wazawa na wawekezaji wa kigeni. Jamii zilizojianda vizuri hupewa kipao mbele zaidi katika mpango mzima, na hu. Na wawekezaji binafsi hugawiwa hadi hekta 5 hadi 10 ya ardhi kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya miti. Utaratibu huo mbali na kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu, kwenye ardhi iliyokuwa haitumiki, lakini unaisaidia serikali kulinda misitu dhidi ya moto, uchomaji mkaa, upotevu wa bioanuwai, uvamizi wa ardhi na shughuli nyngine za binadam. Serikali hukusanya mapato kutokana na ukodishaji ardhi kwa mujibu wa mikataba inayofikiwa na serikali.

Sanduku Na 5. Sera ya taifa ya Misitu ya **Zimbabwe** (2016) *Mojawapo ya mikakati katika sera ya taifa ya Zimbabwe iliyofanyiwa uhakiki ni "* kuendeleza ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza, kuanzisha ,kusimamia mashamba makubwa ya miti kupitia mipango mizuri ya usimamizi na utoaji wa motisha." Mfano wa

Zimbabwe unafurahisha kwa kuhusishwa kwa jamii katika mipango ya Ushikiano wa secta ya umma na sector binafsi/PPP yaani PPCP/Public-Private-Community-Partnerships

Sanduku Na 5. Kauli za Sera ya Taifa ya Misitu ya **Ghana**" Serikali itandaa mifumo na motisha kuendeleza sekta za umma za binafsi na za kijamii kuwekeza katika shughuli za upandaji upya na uanzishaji wa mashamba makubwa ya miti kwenye ardhi chakavu inayofaa kupandwa miti." " Kuendeleza ushirikianao kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kuwekeza katika sekta ya misitu."

Sanduku Na 6. Kauli ya **Sera** ya Taifa ya Misitu ya **Kenya** (2015)

"Upo umuhimu wa kuanzisha mpango wa muda mrefu wa utunzaji wa misitu kwa kuingia mikataba nafuuu na makubaliano ya kushirikiana pamoja na kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ustawishaji wa mshamba makubwa ya miti "

"Serikali itaendeleza sekta binafsi na kushirikisha jamii kuanzisha na kutunza mashamba mapya ya misitu kwenye ardhi inayomilikiwa na umma, watu binafsi au ardhi ya jamii,"

Sanduku Na 7. Kauli ya **Sera** ya Taifa ya Misitu ya. **Nigeria**:

" Serikali na na jamii kwa ujumla zihakikishe haki ya umiliki wa ardhi kwa watu binafsi na wawekezaji kwa kendeleza mashamba ya miti kwa masharti waliyokubaliana."

2.2.2 FASILI YA MISITU KITAIFA

Sera ya Taifa ya Misitu katika rasimu inataja, *msitu kuwa na maana ya ardhi yenye uoto wa asili wenye ukubwa wa angalu ha .05, lenye matawi yaliyosambaa kufikia asilimia 10% au ardhi yenye spishi za miti zenye uwezo wa kusambaza matawi yake kuzidi asilimia 10% na miti hiyo iwe na uwezo wa kufikia urefu wa kimo cha mita 5 inapokuwa imekomaa".* Fasili hii inaelekea kupendekeza kuwa sehemu kubwa ya nchi ya Tanzania imefunikwa na misitu huku ukweli ukibakia kuwa kumekuwa na uharibifu mkubwa wa misitu uliojitokeza hivyo sehemu kubwa ya nchi imejaa vichaka tu na machipukizi ya pili ya misitu yenye thamani ndogo kiuchumi. Hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kurejesha misitu iliyotoweka katika maeneo mengi.

Fasili iliyotajwa inazuia uwekezaji katika mashamba makubwa ya miti husan chini ya taratibu za maendeleo safi (yaani Clean Development Mechanisms/CDM). Maeneo yaliyosheheni vichaka hayawezi kubadlishwa kuwa mashamba makubwa ya miti kwa kuwa tayari ardhi hizo zinafahamika kuw ni misitu tokana na fasili ya hapo juu. Baraza la Forest Stewardship haliwezi kuruhusu ardhi hizo kupandwa miti upya kwa kuwa zinatosheleza fasili ya msitu. Wadau wangependelea fasili hiyo ibadilishwe kwa kuchukua fasili ya UNFCCC, inafasili msitu kuwa na maana ya *"ardhi yenye eneo lipatalo ha 0.5 hadi ha moja yenye matawi yaliyotawanyika kufikia asilimia 10-30, na urefu wa kimo cha mita 2.5."*

Mapendekezo

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya taifa ya misitu:

• Itaandaliwa fasili nzuri ya msitu wa taifa itakayo zingatia matashi ya wadau na kukubalika kwao.

2.2.4 KODI YA ARDHI

Maoni ya wadau

Kwa mara ya mwisho kodi za ardhi zilipanda kutoka Tshs. 200/- hadi kufikia Tshs. 1000/- kwa ekari. Nyongeza hiyo ya kodi, mara tano ya ile ya zamani, ni kubwa mno kwa wapanda miti kibiashara hasa kwa makampuni yanayomiliki maelfu ya hekta ya mashamba makubwa ya miti. Kodi ya ardhi pia inatozwa kwa eneo lote la ardhi linalomilikiwa badala ya eneo lililopandwa miti. Kodi pia hutozwa kwenye kanda za uhifadhi na misitu ya pembezoni kwa mito iliyoachwa kwa ajili ya kuhifadhi bioanuwai. Kwa mashamba ambayo yako katika mamlaka za halmashauri za miji, kodi yake ni kiwango kinachotozwa na mamlaka za miji ambacho ni adhabu kwa wamiliki. Wadau wanafikirii kuwa **kodi za ardhi kwa ajili ya mashamba makubwa ya miti zitathminiwe upya na zipunguzwe ili zitoe motisha kwa wadau wapande miti na zilenge kuleta usawa zaidi kwa wadau.**

Hali ilivyo Tanzania

Shirikisho la African Forestry limeonyesha wasiwasi kuhusu utozwaji wa kodi usio wa haki na usawa, na kutoa pendekezo la kutotozwa kodi maeneo ya misitu yaliyotengwa kwa hifadhi kama motisha kwa wamiliki na wasimamizi wa misitu kuhifadhi maeneo hayo (AF,2016, 2017).

Mapendekezo

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya taifa ya misitu:

- Serikali itarekebisha viwango vya kodi kwa ardhi ya kustwisha mashamba ya miti ili kodi zifanane na zile zinazotozwa kwenye hifadhi za Taifa (national parks) na hifadhi za Wanyama (game reserves) kwa kutambua umuhimu wa mashamba makubwa ya miti katika huhifadhi bioanuwai, kupunguza mmonyoko wa udongo na kuhifadhi vyanzo vya maji.
- Kodi ya ardhi itatozwa tu kwa ardhi inayotumika kibiashara. Ardhi ya hifadhi na ambayo inasubiri kupandwa miti isitozwe kodi.
- Wakulima wadogo wa miti wasitozwe kodi yoyote hadi watakapokuwa wamevuna miti yao kwa nia ya kuwapunguzia mzigo wa malipo.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Mamlaka ya Misitu ya Serikali ya Uganda inatoza kodi ya ardhi kwa misitu ya serikaly iliyokodishwa kwa wekezaji kati ya UG Shs 8000 kwa ardhi iliyo Km 50 na zaidi nje ya Kampala, na UG Shs 30,000 ndani ya Km 50 kutoka Kampala.

2.2.4 UZUIAJI WA MOTO

Maoni ya wadau

Mioto ya mwituni imeendelea kuwa tishio kwa mashamba makubwa na madogo ya miti nchini. Inabidi kuandaa mikakati ya kuhakikisha hasara zinazotokana na moto zinapungua kabisa. Hakuna mpango wa pamoja wa kudhibiti moto, na mfumo wa kung'amua matukio ya moto na kuzima moto hapa nchini hautoshelezi kabisa. Vikosi vya moto vya Manispaa hutoza gharama za juu sana, kiasi cha Tshs million 2 kwa kila hekta moja kuzima moto. Fedha hizo ni nyingi mno kwa wakulima wa miti wadogo na wa kati. Washika dau wanafikiri kuwa **Sera ya Taifa ya Misitu ihakikishe vijiji hadi ngazi ya Taifa kunakuwepo uwezo mkubwa wa kuzuia, kupunguza na kudhibiti moto ikizingatiwa kuwa moto ni adui mkubwa dhidi ya utunzaji na usimamizi wa mashamba ya miti.**

Hali ilivyo Tanzania

Moto wa mwituni ni tataizo kumbwa linalo yakumba mashamba makubwa ya miti cnhini Tanzania. Kati ya mwaka 2005 hadi 2009, karibu ya hekta 6,000 ziliteketea kwa moto, sehemu kubwa ikiwa katika shamba kubwa la serikali la Sao Hill (hekta 2,160) na Kilombero Teak Valley (hekta 3,300). Na mwaka 2009/10, jumla ya hekta 3,900 ziliathiriwa kwa moto (Kiangi, 2010; Mussami, 2010). Taarifa za hivi karibuni za waandaaji miongozo jumuishi ya kudhibiti matukio ya moto Tanzania, miongozo hiyo inahitajika kwa haraka sana kwa sababu ya upanuzi mkubwa wa mashamba ya miti hasa Nyanda za juu Kusini. Ukosefu wa mipango ya uwekezaji katika sekta ya misitu hufanya uandaaji wa mkakati wa kupambana na moto kuwa mgumu. Mapitio ya sera mpya ya Taifa ya misitu inelekeza haja ya uelewano kati ya sera mbalimbali kwani matumizi ya moto hutumika kwenye kilimo kusafisha mashamba, na pia kuna matumizi ya moto katika mbuga za wanyama na mapori ya akiba.

Mapendekezo

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya taifa ya misitu:

- **Serikali kwa kushirikiana na vyombo husika itaanzisha shirika la kusimamia kitaifa moto wa mwituni, kwa madhumuni ya kuwa na mpangilio mzuri wa kufuatia, kugundua, kuzuia na kuzima moto.**
- **Mafunzo juu ya udhibiti wa moto kichaa yataandaliwa kuanzia ngazi ya kijiji, na ngazi ya Wilaya kwa kushirikiana na sekta binafsi na washika dau wengineo.**
- **Halmashauri za Wilaya zitavigawia vikosi vya kuzima moto, vifaa na zana muhimu.**
- **Sheria zinazohusiana na uchomaji moto zitapitiwa upya na kufanyiwa marekebisho yenye kuleta matokeo yanayotakiwa.**

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na 8. Usimamizi shirikishi wa kudhibiti moto **Afrika ya Kusini.** Tujifunze kutoka Afrika ya Kusini ambako Serikali na sekta binafsi wameunda mfumo madhubuti wa kufuatia na kuzima mioto ya mwituni. Vikosi maalum vimepewa mafunzo ya kushughulikia matukio ya moto wa mwituni kwa kushirikiana na majeshi ambayo yanakaa yakiwa yamejiaandaa kwa matukio ya moto wakati wowote.

2.2.5 WADUDU WAHARIBIFU NA MAGONJWA

Maoni ya wadau

Ingawa nchi ina bahati kubwa kwa mashamba ya miti yake kutoathiriwa na magonjwa au kushambuliwa na wadudu waharibifu, ambapo matukio machache tu yamewahi kutokea (k.m. cypress aphid, woolly aphids, Eucalyptus chalcid), bado hakuna uhakika kwamba hayatajitokeza siku zijazo. Hivyo Wadau wanashauri **Sera ya Taifa ya Misitu Ihakikishe nchi inakuwa na uwezo mkubwa wa kutambua na kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu kwa kuwa ni hatari kubwa kwa mustakabali wa ustawi wa misitu yetu.**

Hali ilivyo Tanzania

Mashamba ya miti nchini Tanzania yamewahi kukumbwa na wadudu waharibifu, hususan kuangamizwa mashamba makubwa ya miti aina ya cypress. Ushahidi kutoka nchi nyingine unaonyesha kuwepo kwa ueneaji wa wadudu waharibifu na magonjwa, na inatarajiwa hali hiyo kuongeza athari zake nchini Tanzania, ikizingatiwa kuwa mabadliko ya tabia nchi yaweza kuongeza usambaaji wa matukio hayo. Taasisi ya TAFORI inalo jukumu la kupambana na wadudu waharibifu na magonjwa, lakini wana uwezo mdogo sana wa kutambua na kuchukua hatua stahiki katika ngazi zake zote.

Mapendekezo

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya Taifa ya Misitu:

- **Serikali itaanzisha kitengo cha kitaifa cha kufuatilia na kudhibiti matukio ya wadudu waharibifu na magonjwa ambacho kina mfumo imara wa kusambaza taarifa, na chenye uwepo kote nchini.**
- **Serikali itaimarisha utafiti wa wadudu waharibifu na magonjwa kwenye taasisi zote za utafiti na vyuo vikuu**
- **Wakulima wa miti na wakulima wa mazao ya chakula watapewa mafunzo juu ya kutambua wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea.**

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Afrika ya Kusini na Zimbabwe zimeonyesha kuwa, udhibiti wa wadudu waharibifu kwa mbinu mchanganyiko na kuzalisha miti inayostahimili maradhi ni ufumbuzi mmojawapo wa kupunguza changamoto za wadudu waharibifu na magonjwa.

Sanduku No 9. Mpango shirikishi wa kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa**-- Afrika ya Kusini**Ushirika wa kinga ya maradhi na wadudu waharibifu dhidi ya miti uliundwa kwa ushirikiano kati ya washika dau wakiwemo sekta binafsi, serikali na taasisi za utafiti huko Afrika ya Kusini. Ushirika huo hutekeleza majukumu yake kwa ushirikiano wa karibu sana na Centre for Excellence in Tree Health Biotechnology chini ya mwamvuli wa Forest and Agricultural Biotechnology Institute (FABI). Taasisi hiyo hufuatia uwepo wa hatari yoyote inayoweza kusababishwa na magonjwa au wadudu waharibifu, na kwa kupitia tafiti zake na kushirikiana kimataifa, chuo hicho huandaa mbinu za kuzima vitisho vya uharibifu uanoweza kutokea.

2.2.6 UZALISHAJI WA MITI YENYE UBORA NA VIFAA VYA KUSTAWISHIA MITI

Mawazo ya wadau

Sekta ya upandaji miti kibiashara imekumbwa na tatizo la kupanda miche yenye ubora mdogo kutoka katika aina chache sana za miti ya kibiashara. Sekta imekuwa ikitegemea kupanda aina chache za misindano na mikaratusi. Ukosefu huo wa aina nyingi na bora za miti ya kupanda umeathiri uzalishaji na ubora wa mashamba ya miti, na umesababisha uagizaji kufanyika nje ya nchi li kupata mbegu zenye ubora kwa nia ya kupata mazao yaliyo bora zaidi na hatimaye kuvuna mazao timbao bora. Utegemezi wa kustawisha aina chache ni hatari endapo utajitokeza mlipuko wa maradhi. Washika dau wanashauri **Sera ya Taifa ya Misitu kuzingatia kuwa juhudi za washika dau za utafiti wa kuboresha miti ya kupanda uliopo kwa sasa, unapatiwa fedha za kutosha na kuratibiwa inavyostahili ili uwe endelevu, na ili kuhakikisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora kwa kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kwenye uzalishaji na usambazaji.**

Hali ilivyo Tanzania

Ushikishwaji wa kuboresha miti ya kupanda ulianzishwa na Idara ya Misitu mwaka 2013, Nyanda za juu Kusini.Kikundi shirikishi cha sekta ya umma na sekta binafsi cha Utafiti wa Kuboresha Miti (Tree Improvement Research Working Group) kilianzishwa, na kikatengeneza mkakati wa kuboresha miti katika nyanda za juu kusini. Hali hiyo imewezesha kufanyika kwa majaribio mengi ya kuchunguza aina za miti zinazoweza kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali ya Nyanda za juu Kusini. Majaribio ya vizazi bora (breeding populations) yameanziswa kwa jamii mbili kuu za miti zinazopandwa katika nyanda za juu kusini. Inatarajiwa majaribio yayatakayofanyika yatatoa taarifa za kuwezesha uingizaji kutoka nje wa aina za miti mbadala. Mipango inaandaliwa ya kuanzisha mashamba ya mbegu (seed orchards) na vipandikizi (clones) vya kustawisha Mikaratusi na Misindano kwa madhumuni ya kupata mbegu bora. Ili kupata mbegu bora za miti zenye kuhimili kwa kipindi kirefu, kampuni ya mbegu imeanza kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi na kuzisambaza kwa wakulima wa miti.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika mswaada- jaribio wa sera ya Taifa ya Misitu:

- **Serikali itaongeza mafungu ya fedha kwa ajili ya utafiti wa wa kuongeza obora wa miti pamoja na kujenga uwezo zaidi wa kutafiti**
- **Serikali itaendelea kutoa ushauri kuhusu matumizi ya mbegu bora na miche iliyo bora na kutoa ruzuku kuwezesha uingizaji wa mbegu bora na pembejeo zinazohitajika kutoka nje**
- **serikali itaisaidia sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuzalisha na kusambaza mbegu bora nchini kulifanya taifa kujitegemea kwa uzalishaji wa mbegu bora za miti.**

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na10. Jukumu la sekta binafsi kusambaza mbegu**---Nigeria** " Sekta binafsi ina jukumu kubwa la kukusanya na kusambaza mbegu za miti na miche ya kupanda. Serikali itasaidia kujenga uwezo wa sekta binafsi ili sekta hiyo ifikie uwezo wa kuuza na kusambaza mbegu, na udhibiti wa ubora wake. Kujenga uwezo wa kusambaza mbegu kwa kutumia sekta binfsi. Kuhakikisha mahitaji maaluum ya mbegu kwa kila kanda ya kiikolojia nchini shughuli za usimamizi wa vitalu vya miche yanafikiwa na kutekelezwa. Kuanzishwa kwa mashamba vya kuzalisha mbegu (seed orchards) na ya kuhifadhi uasili wa mbegu (seed banks). Kutia moyo uzalishaji wa mbegu, miche na aina za miti ya asili."

2.2.7 UPASHAJI HABARI NA SHUGHULI ZA UGANI

Maoni ya washikadau

Utendaji wa watumishi wa serikali wa ugani umeshuka kwa kiwango cha juu hapa nchini na uepo wa maafisa ugani hauonekani kwa wahitaji. Hali hiyo imejitokeza kipindi ambacho unahitajika uangalifu mkubwa katika kuingiza mbegu bora mpya za miti pamoja na kuwaongoza na kuwafundisha wakulima wa miti, waandaji wa vitalu kuhusiana na usimamizi mzuri na kuwawezesha kupata mazao bora.

Washikadau wanafikiria Sera ya Taifa ya Misitu ihakikishe Serikali inakiimarisha na kukiongezea uwezo kitengo cha ugani wa misitu kwa kukiongezea fedha na wafanya kazi bora.

Hali ilivyo Tanzania

Kanuni za ustawishaji wa mashamba ya miti na usimamizi wake umekwisha kutolewa na Wizara ya Mali Asili na Utalii (FBD, 2017), pamoja na kusambaza picha za video na vipeperushi katika lugha ya Kiswahili. Mafunzo juu ya utunzaji wa vitalu na uanzishwaji wa mashamba ya miti yamekuwa yakitolewa na serikali, sekta binafsi na programu za FDT na PFP. Programu ya Panda Miti kibiashara imeunda vikundi vya wakulima wa miti chini ya uongozi wa juu wa chama cha wakulima wa miti. Vikundi vya wakulima wa miti vinategemewa kutoa huduma za ugani kwa wanachama wake, ili mradi tu vikundi hivyo vitawezeshwa kufanya hivyo.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika mswaada- jaribio wa sera ya Taifa ya Misitu:

- **Serikali itaimarisha huduma ya ugani na kuwawezesha wafanyakazi kupata vifaa vya kufanyia kazi na ujuzi unaohitajika kutimiza majukumu yao ipasavyo.**
- **Serikali itahakikisha huduma za ugani zinwafikia wananchi walioko vijijini ambako ndiko zinakofanyika shughuli za ustawishaji wa miti. Vyama vya wakulima wa miti vitaimarishwa kwa kuongezewa ujuzi, maarifa na vifaa vinavyohitajika kwa shughuli za ugani.**

Uzoefu kutoka nje ya nchi

Sera ya Misitu ya Uganda inaunga mkono kwa dhati shughuli za ugani wa misitu (Sanduku Na 11)

Sanduku Na 11: Lengo na mkakati wa **Uganda** kuunga mkono shughuli za kilimo cha miti:"Kilimo cha miti kitatiliwa mkazo katika aina zote za kilimo na mbinu mpya za kutoaelimu na ushauri kwa njia ya ugani zitaendelezwa ipasavyo Serikali itatoa huduma zaugani na ushauri zitakazowasadia wakulima, wanajamii, mashirika na wafanya biasharakuhifadhi na kusimamia misitu ipasavyo na maendeleo ya kilimo cha miti. Serikali inatambua kuwa kuna mahitaji makubwa kuhusu ushauri wa kilimo cha miti karibu nchi nzima, na umuhimu wa kupata huduma za watatalaam wa misitu. Hudumahizo zitaendelezwa kitaifa na zitahusu zaidi utetezi, na ufuatiliaji wa Wizara inayohusika na shughuli za misitu na itatoa huduma kupitia kwa wakulima wenyewe ili kuongeza kufungamana kwa shughuli za kilimo cha miti na mikakati ya kuwaongezea kipato wananchi wa vijijini."

2.3 MASWALA YA KISERA KUHUSIANA NA UENDELEZAJI WA VIWANDA VYA MISITU

2.3.1 UPATIKANAJI WA MALI GHAFI

Mawazo ya washikadau

Upo uhaba mkubwa wa malighafi zinazopatikana kutoka kweny mashamba ya miti ya serikali kuweza kuendesha viwanda vya kupasua mbao na kuvutia uwekezaji katika mashine zenye ufanisi mkubwa. Hali hii hutokana na malihgafi za ubora wa chini, upungufu wa magogo, na ugawaji wa bloko za mashamba ya miti usiokuwa wa uwazi. Washikadau wanafikiri **Sera ya Taifa ya Misitu hakikishe inaandaa mipango ya muda mrefu ya upatikanaji wa malighafi ili wawekezaji wawe na uhakika wa upatikanaji wa malighafi kwa wingi na yenye ubora unaohitajika.**

Hali ilivyo Tanzania

Kihistoria, mashamba ya serikali hayakutunzwa kwa ufanisi. Mbegu na miche ya miti vimekuwa na ubora hafifu, na shughuli nyingi za utunzaji wa mashamba ya miti zimekuwa hazifanyiki. Matokeo yake yamekuwa ni uzalishaji usiotosheleza na ubora cha chini wa malighafi za viwanda (URT, 1998). Hali hiyo ikichanganywa na pengo liliokuwepo la kutoendelea kupanda mashamba ya serikali, hadi hivi karibuni, kuna upungufu mkubwa wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya misitu. Hili limepelekea biwanda vingi vya kupasua mbao kuzalisha chini ya aslimia 40-50% ya uwezo wao (Indufor, 2011). Katika Msitu wa kupandwa wa Sao Hill, kiasi cha magogo yanayostahili kuvunwa kimeshuka kutoka mita za ujazo milioni 1.2 kwa mwaka kipindi cha 2005 hadi kufikia mita za ujazo 700,000 kwa mwaka hvi sasa. Vibali vilivyotolewa kwa ajili ya uvunaji wa kiwango hicho cha magogo vilifikia 964. Wenye viwanda ambao wana mikataba ya muda mrefu na Wizara walitengewa asilimia 60% katika mwaka wa fedha wa 2015/16 na kiasi kilichobaki kilitengwa kwa wajasiriamali wapatao 800, wengi wao akiambulia mita za ujazo 200 tu za miti iliyosimama. Kwa kugawiwa kiwango hicho mfanya biashara huyo ataweza kuendesha kiwanda chake kwa miezi 2 tu katika mwaka mzima (PFP, 2016).

Mfumo wa ugawaji wa magogo umetoa nafasi kwa madalali wa kati (wenye viwanda vya mbao vya mfukoni) kupewa vibali vya uvunaji wa magogo kwa njia zenye kutatanisha, wakiwa na lengo ya kuuza mgao huo kwa bei kubwa zaidi. Watu wa aina hiyo huchukulia uhaba wa malighafi ya timbao kama fursa ya kuuza mgao wao wa sehemu ya msitu kwa bei ya juu sana, hali ambayo inaongeza sana bei ya mbao sokoni. Mashamba ya watu binafsi ndiyo yatakayotegemewa kuvipatia viwanda malighafi ya timbao siku za usoni. Hata hivyo mengi ya mashamba binafsi hayana mipango ya usimamizi na yanavunwa kabla ya miti kukomaa ipasavyo kukidhi changamoto za kaya. PFP (2016) walipendekeza kuwa, kila shamba la mkulima liandaliwe mpango wa kutunza mashamba ili kuhakikisha miti inavunwa ikiwa imekomaa. Pia iwawezeshe wakulima hao kukisia viwango vya ujazo wa magogo utakaopatikana na hivyo kupanga mkakati wa upatikanaji wa masoko.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika mswaada- jaribio wa Sera ya Taifa ya Misitu:

● **Wizara ya Maliasili na Utalii itavikagua upya viwanda vyote vya misitu kulingana na uweza na ufanisi wao wa kuzalisha ili kubaini vile vinavyokizi vigezo ndio vipewe leseni. Hivyo ndio viwanda**

vitakavyopewa magogo ya malighafi ya kutosha kutoka kwenye mashamba ya serikali ili vizalishe kwa uwezo wake wote mwaka mzima. Viwanda vilivyoteuliwa vitauziwa magogo na kupewa leseni kwa kipindi cha kati ya miaka 3-5 kuviwezesha viwanda kupanga uzalishaji, uuzaji na uendeshaji kifedha wenye ufanisi

● Serikali itakuwa inafanya tathmini ya wingi na ubora wa magogo kwenye mashamba yake na mashamba binafsi na kutumia taarifa zitakazopatikana kupima mahitaji halisi ya viwanda dhidi ya mahitaji kitaifa ya timbao. Taarifa hizo zitasambazwa kwa washika dau.

● Serikali itahimiza upandaji miti na utunzaji wa mashamba nchi nzima, kwa madhumuni ya kuinua viwango vya ubora, uzalishaji na kuondoa upungufu wa magogo viwandani. Washika dau wote (TFS, sekta binafsi, na wakulima wa miti wadogo na kati) watahusika na zoezi hili.

● Serikali itahimiza ufanisi katika uvunaji wa magogo na uzalishaji wa bidhaa zake ikiwepo uongezaji wa thamani na matumizi ya mabaki kwa tija.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na 12: Lengo la **Uganda** kuhusu mkakati wa kuunga mkono viwanda vya uchakataji wa mazao ya timbao

“Serikali itasaidia sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kisasa, vyenye ushindani, nyenye ufanisi wa juu, na vilivyothibitishwa; Sekta binafsi itawajibika kuviendesha na kuviendeleza viwanda kuchakata mazao ya timbao na kuviwezesha viwanda hivyo kuongeza thamani ya mazao.

Ni wajibu wa serikali kuwezesha na kusimamia shughuli hizo. Serikali itaanzisha mfumo wenye nguvu wa kudhibiti vitendo visivyofuata sheria, kufuatilia utendaji stahiki, kupima athari za mazingira, na kukusanya ushuru: Serikali pia itaweka mazingira mazuri kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya timbao. Mkakati wa utekelzaji wa matamko hayo ya Sera yatahusisha:

● Kuanzisha zabuni za ushindanishi kwa ajili ya kupewa hati milki ya uvunaji katika mashamba ya serikali, kuongeza uwazi, mapato ya serikali, kuonyesha uhalisia wa thamani ya mazao timbao yanayopatikana.

● Kuanzisha mikataba fungamo ya makandarasi wa uvunaji ili kuboresha utendaji na usimamizi unaofaa.

● Kuboresha kanuni za mikataba ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwango vya uvunaji, tathimini ya athari kwa mazingira, na ukusanyaji maduhuli ya serikali.

● Kusawazisha viwango vya ushuru vinavyozingtia hali ya uchumi wa rasilimali za misitu nchini, wakati huo huo vitikwatia motisha wawekezaji. "

2.3.2 MAZAO YA VIWANDA NA UFANISI

Maoni ya washikadau

Viwanda vya misitu vimesheheni na vifaa na mitambo ya zamani iliyochoka. Matumizi ya tekinolojia duni husababisha uzalishaji wa bidhaa za timbao duni pia, kama utoaji wa mbao zisizokidhi viwango. Washikadau wanafikiri kuwa **Sera ya Taifa ya Misitu -tarajiwa utoe vivutio na uwezeshaji wa kiteknolojia wa kuviwezesha viwanda vya misitu kubadilisha uzalishaji kuelekea tekinolojia yenye ufanisi mkubwa zaidi**.

Hali ilivyo Tanzania

Asilimia 78% ya teknologia ya upasuaji mbao nyanda za juu kusini ni ya chini mno. Mashine za kuhamahama za kupasua mbao zinazokadiliwa kufanya aslimia 51% ya viwanda vyote vya kupasua mbao katika mashamba ya serikali (PFP, 2016) ni zenye teknolojia ya chini pia. Tekinolojia hiyo ina uwezo wa kiasi cha kinachofikia kati ya asilimia 25-35% ya upatikanaji mbao ikilinganishwa na tekinolojia mpya yenye kutoa upatikanji wa mbao wa kati ya aslimia 38- 40%. Viwango vya chini vya upatikanaji wa mbao kwa mashine za kuhama hama ukilinganisha na upatikanaji wa mbao wa aslimia 50 inapotumika misumeno bora, husababishwa na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara mashine na vifaa vyake.

Serikali inafanya juhudi ya kubadilisha teknolojia katika viwanda vya misitu ili kuinua ufanisi wa uzalishaji viwandani. Kanuni mpya zilizowekwa na serikali zinazuia kupeleka magogo yakapasuliwe kwenye mashine za kuhamahama ambazo husababisha upotevu mkubwa wa mbao na ni hatari kuziendesha. Misumeno yenye ufanisi mkubwa (circular and band saws) ndiyo inayopendekezwa kutumika badala ya mashine za kuhamahama (Ding Dongs). Ufufuaji upya wa vifaa vya kupasua mbao unafanyika kwa kutumia tekinologia ya misumeno ya kutoka India, China, na Marekani. Mradi wa Panda miti Kibiashara una mpango wa kuweka mashine 2-3 za kupasua mbao zilizo bora katika Nyanda za juu Kusini, kwa ajili ya mafunzo ya technolojia fanisi za upasuaji wa mbao. Madhumuni yake ni kuinua ufanisi na teknolojia za upasuaji wa mbao. Ubadilishaji wa tekinolojia viwandani kunahitaji maarifa ya kutambua mashine zinazofaa kwa kuzingatia mazingira ya vijijini na upatikanaji na usambazaji wa vipuri na upatikanaji wa mafundi wenye ujuzi wa kufanya matengenezo Kuna uhaba mkubwa wa mafundi mchundo na mafundi stadi wa kufanya kazi viwandani. Mafunzo yanayotolewa kwenye Vyuo vya Ufundi Stadi hayafanani na changamoto za kiufundi za viwanda vya misitu. Ili kuziba pengo hilo Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) viianzishe kozi zinazohusiana na uendeshaji wa viwannda vya misitu katika mitaala yake. Na wanafunzi wa vyuo hivyo watumie muda mwingi wa mafunzo kwa vitendo.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya Taifa ya Misitu:

- Serikali itatoa ushauri wa kiufundi stahiki kwa makampuni ya biashara ya misitu madogo na ya kati kuhusiana na manunuzi yam ashine za teknologia sahihi kwa uendeshaji wa viwanda kwa ufanisi zaidi.
- Wizara ya Maliasili na Utalii itashirikiana na taasisi husika za serikali kuanzisha mafunzo yahusuyo viwanda vya misitu kwenye Vyuo vya Ufundi Stadi kwa ngazi ya cheti na ya stashahada ili kuondoa hali iliyopo ya upongufu mkubwa wa mafundi katika sekta ya misitu.
- Wizara inatambua na kuunga mkono juhudi za Programu ya Panda Miti Kibiashara kuanzisha mafunzo

ya kiufundi katika mitaala ya Chuo cha Mafunzo ya Viwanda vya Misitu, na Vyuo vya Ufundi Stadi

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na 13: Mikakati ya **Uganda** ya kuunga mkono viwanda vya kuchakata mazao ya timbao

● Kuongeza ufanisi na kupunguza upotevu wa timbao kwa kutumia mashine stahili, kufanya utafiti, na kutumia teknolojia mpya. Kuongeza ongezeko la thamani ya bidhaa kwa kupunguza uuzwaji nje wa malighafi na kutoa mazao ya timbao ya hali ya juu kwa hatua zote za uchakataji

● Kuongeza mazao na masoko mapya ya mazao ya timbao na yasiyo ya timbao.

2.3.3 BIASHARA NA MASOKO YA TIMBAO

Hali ilivyo Tanzania

Masoko dhaifu na viwanda vya zamani kunarudisha nyuma maendeleo ya ustawishaji wa mashamba makubwa ya miti (Indufor 2011). Mazao yasiyokuwa na ubora yasiyoweza kuuzwa kwa bei nzuri, ni mojawapo ya sababu zinazowakatisha tamaa wawekezaji na wakulima wa miti kupanua mashamba. Hali hiyo ni mbaya zaidi kwa sababu ya ukosefu wa taarifa za masoko za kuwaelekeza wenye viwanda na wanunuzi wakubwa. Takwimu za hali ya biashara nchini Tanzania zimesambaa mno na ni za kuwachanganya wafanya biashara (Mwamakimbullah, 2015).

Mashamba makubwa ya miti hutoa magogo yenye ujazo mdogo yasiyokidhi mahitaji ya soko na hayana ubora unaohitajika kwenye soko la ndani na la nje. Kwa hali hiyo bidhaa zetu haziwezi kuhimili ushindani.

Kuna umuhimu wa kuweka viwango vya mazao ya timbao muhimu kwa soko la ndani na la nje. Shirika la Viwango Tanzania limetoa viwango kadhaa vya mbao ambavyo vinapatikana kwenye tovuti ya shirika hilo. Mifano ya viwango vichache imeorodheshwa hapa chini:

a) TZS 81:2009, Paper and board - Determination of grammage;
b) TZS 256: (Part 1) 2009, Timber - Determination for coniferous sawn timber (cypress and pine) - Part 1: Sizes of sawn and planed timber;
c) TZS 657: 2011, Glossary of terms used in timber industry;
d) TZS 661: 2011, Copper/chromium/arsenic composition for the preservation of timber - Methods for timber treatment; and
e) TZS 686: 2011, Wood poles and blocks for power and telecommunication lines - Specification.

Baadhi ya viwango hivi havitoshelezi bali vinatakiwa kufanyiwa marekebisho makubwa kwa kuwa vimeangaliwa viwango vichache tu. Wizara ya Maliasili na Utalii wanatakiwa kufanya kazi kwa pamoja na Shirika la Viwango Tanzania kuandaa viwango vilivyobakia na kuboresha vilivyopo. Viwango vilivyopo kwa sasa ni kwa mbao zinazosafirishwa nje lakini viwango kwa soko la ndani havipo. Na hakuna viwango vinavyohusu magogo, jambo linalohitajika kupatiwa ufumbuzi haraka. Viwango vilivyopo na vitakavyoandaliwa upya vilinganishwe na kufanana na viwango vinavyotumika kimataifa (COMESA, SADC na EAC). Uvunaji wa magogo bila vibali na biashara ya magendo wa mazao ya timbao nje ya mipaka ya nchi ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazoharibu bei za masoko.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya Taifa ya Misitu:

- **Serikali ikomeshe biashara ya magendo ya mazao ya timbao kwa kuanzisha mtandao wa kufuatilia mazao hayo yanakopatikana hadi kufikishwa soko la ndani au la nje;**
- **Serikali itasimamia uanzishwaji wa mnada wa mbao**
- **Serikali itaandaa kanuni na kusimamia utaratibu wa kupima na kuhakiki viwango ili mazao yanayokidhi viwango au kuzidi viwango vilivyowekwa ndiyo yaruhusiwe kupelekwa sokoni.**
- **Serikali itawezesha tafiti za masoko, na kuchambua na kusambaza taarifa za masoko na fursa zilizopo za kufanya biashara ya mazao ya timbao hapa nchini na nje ya nchi.**

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na 14: Matamko ya Sera **Kenya** – mnyoro wa bidhaa" **Kuanzisha na kusimamia mnyororo wa bidhaa wa kitaifa ili kufuatilia usafirishaji wa mazao ya timbao kwa ajili ya masoko la ndani na nje."**

Sanduku Na 15: **Matamshi ya Sera ya Nigeria** – kuyapanga mazao ya timbao katika madaraja na ufuatiliaji " Kuanzisha kanuni za upangaji wa mazao ya timbao katika madaraja na kuzitumia kanuni hizo kuhakikisha uzalishaji wa timbao zilizo ongezwa thamani zinakubalika katika masoko ya ndani na nje.Kuanzisha utoaji wa hati za uthibitisho wa Usimamizi Endelevu wa Misitu (Sustainable Forest Management/SFM*)* unaojumuisha ufuatiliaji wa magogo ili kuhakiki kukubalika kwa mazao ya timbao katika masoko ya ndani na nje."

Sanduku Na16: Matamshi ya Sera ya **Zimbabwe – hati za uthibitisho"**. Kusisitiza na kukubali kusanifisha utaratibu wa hati za uthibitishoo wa mazao ya timbao ili kuongeza ushindani kwa bidhaa za mazao ya timbao ya Zimbabwe kukubalika kimataifa na ndani ya ukanda wa SADC"

2.3.4 UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA KIBIASHARA KWA MAZAO YA TIMBAO

Maoni ya washikadau na hali ilivyo tanzania

Washika dau wanafikiri ziko changamoto nyingi ambazo si rafiki kwa mazingira ya kufanya biashara:

Kuunganishwa kwa tozo za leseni ya misitu na tozo nyingine mbalimbali: Kwa kipindi hiki serikali imekuwa ikitoza kodi na tozo zifuatazo: tozo kadirio (Assessment fee); Ada ya usajili (Wood products trade registration) kwa mwuzaji na msambazaji; Ushuru wa usafirishaji (Transit passes); ushuru wa halmashauri ya wilaya (District Council Cecc); Kodi ya Ongezeko la Thamani (Vallue Added Tax/VAT); LMDA na Ushuru wa TFF (Idara ya Misitu na Nyuki) /TFF Levy. Tozo zote hizi zimeonekana kuwa kwa ujumla wake ni kubwa mno kiasi cha kuzifanya bei za mbao kuwa za juu sana na kutoweza kuhimili ushindani sokoni. Kodi hizo zinatakiwa zipitiwe upya na hasa tozo la VAT kwa miti ambayo haijavunwa. VAT itozwe kwa mazao ambayo yamekwisha chakatwa badala ya kutoza VAT kwa malighafi.

Vizuizi vya TFS, Vizuizi vya Polisi na Mizani huchelewesha mfumo mzima wa usafirishaji na kuongeza gharama. Magari yanaweza kufunga safari 1-2 kwa wiki kutoka Mafinga hadi Dar es Salaam badala ya safari 3-4 kabla ya kuwekwa vizuizi vingi namna hiyo. Serikali imetoa mwongozo wa kuzuia kusafirisha mazao ya misitu wakati wa usiku jambo hili linapunguza ujazo wa bidhaa zinazoingia sokoni.

Wizara ya Maliasili na Utalii imeongeza kanuni nyingine kwa kuwataka wafanya biashara wanaohitaji kupeleka mbao sokoni kusajiliwa na TFS. Na msambazaji naye sharti asajiliwe pia. Nakala halisi na picha za mfanya biashara na msambazaji, ni lazima ziambatanishwe na kila shehena ya mbao inayopelekwa sokoni. Utaratibu huu unasababisha usumbufu mkubwa ambao hata vi vigumu kuusimulia. Kwa maana mfanya biashara analazimika kutumia gari moja kwa wakati mmoja. Endapo mfanyabiashara atashindwa kuelewana hapo baadaye na msambazaji, itakuwa vigumu kwa mfanya biashara huyo kumwuzia msambazaji tofauti na yule wa kwanza, kutokana na taratibu hizo mpya.

Mapendekezo

● Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika mswaada- jaribio wa sera ya Taifa ya Misitu:
● Wizara ya Mali Asili na Utalii itazifanyia marekebisho kanuni na sheria zote zinazohusiana na uendeshaji wa viwanda vya misitu na kuondoa vikwazo vyote vya kibiashara ili kurahisiha biashara ya mazao ya mitimbao na kuuboresha ushindani wa kibiashara.

● Serikali itazifanyia marekebisho kodi zote zinazotozwa na sekta ya misitu, hii ni pamoja na vibali vyote vya ushuru, vibali, leseni na sesi (ada ya halmashauri) ili kupunguza urasimu. Serikali itarekebisha kodi na tozo nyingine ili kuyafanya mazao timbao yaweze kuwa ya ushindani katika masoko ya ndani na nje.

● Wizara ya Mali asili na Utalii itawasaidia wafanya biashara wa mazao ya mitimbao kukuza kibiashara kwa kuweka wazi taarifa za masoko na kulea Bishara ndogo ndogo na za kati kwa kutoa mafunzo ya undeshaji na usimamizi wa maendeleo ya biashara.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku Na 17. Sera ya Misitu ya **Uganda** - wajibu wa serikali wa kuandaa mazingira mazuri yakufanya biashara " Wajibu wa serikali utakuwa ni kuunga mkono na kusimamia maendeleo hayaya biashara. Itaweka kanuni za kudhibiti vitendo vitakavyofanywa kinyume cha sheria, kufuatia taratibu nzuri, kupima matokeo na athari za mazingira na za kijamii na ukusanyaji ushuru. Serikalia itweka mazingira mazuri ya kuwavutia wakezaji binfsi katika kuanzisha mashamba makubwa ya miti."

2.4. MAZINGIRA BORA YA KUVIWEZESHA VIWANDA

2.4.1 URATIBU WA SEKTA BINAFSI NA UBADILISHANAJI WA MAONI

Maoni ya Wadau

Nchini Tanzania sekta binafsi ya panda miti kibiashara haina mfumo mzuri na inakosa utaratibu wa uongozi thabiti wa kuwezesha ukusanyaji wa maoni mbalimbali na uwakilishi kisekta. Sekta binafsi ya panda miti kibiashara iko katika ngazi ya mwanzo kabisa, inahitaji kulelewa na kutunzwa ili iweze kuwa yenye nguvu na yenye mfumo imara kauchangia katika kukuza uchumi kitaifa. Kwa hali hiyo inahitajika kuendeleza mifumo inayozingatia kuwepo kwa wadau wa aina nyingi pamoja na wafanya biashara wadogo wasiokuwa kwenye mfumo maalum. Mikutano kati ya serikali na wadau ni ya nadra kufanyika. Matokeo yake kila mdau hufanya maamuzi bila kumshirikisha yeyeote. Wadau wanafikiria kuwa **Sera ya TAIFA YA Misitu inapaswa kiimarisha utaratibu kwa kuihusisha sekta binafsi na kuanzisha mashauriano na midahalo juu ya mambo yanahusiana na sekta binafsi ya panda miti kibiashara.**

Hali ilivyo Tanzania

Sekta binafsi ya misitu nchini Tanzania kwa sasa inawakilishwa na vyama mbalimbali kama SAFIA (Southern Forest Industries Association), NOFIA (Northern Forest Industries Association), UWAMBU (Umoja wa Wavunaji Miti Buhindi), UWASA Umoja wa Wavunaji Sao Hill) na SHIVIMITA (Federation of Timber Industries Association) kama chombo cha juu cha uwakilishi. Vipo pia vyama viwili vinavyojishughulisha na wakulima wa miti na makampuni yenye mashamba makubwa ya miti. Vyama hivyo ni Tanzania Tree Growers Association na African Forestry Tanzania. Vyama hivyo ni dhaifu na havina uwezo wa kuwakilisha mawazo ya kisekta.

Mwanakimbullah (2016) alipendekeza muundo wa sekta binafsi Tanzania (Kielelezo Na. 1) Kipeo cha uongozi wa mfumo huo kikijumuisha Tanzania Sawmillers Association, Tanzania Wood Preservers Association, Tanzania Tree Growers Association. Tofauti na hivyo vyama inaweza kuhakikisha kuwa wanachama wenye uwezo mdogo, wa kati na wakubwa wanaingizwa katika uongozi wa juu wa ushirika wa vyama vilivyotajwa hapo juu. Kila chama kitaunda kamati mbalimbali za kushughuhulikia mambo tofauti k.m. usawa wa kijinsia katika chama cha wakulima wa miti.

Kwa kuongezea, baraza litahitajika pale ambapo sekta binafsi ya sekta ya miti itahitajika kufanya majadiliano na serikali ya pande zote mbili. Kwenye baraza hilo serikali itatangaza sera zake na sekta binafsi itawasilisha shughuli zao za biashara na uendeshaji. Majadiliano ya pande hizo mbili yatakuwa na lengo la kuwa na maelewano yenye usawa.

Kwa kutekeleza shughuli za kila siku za muundo wa bodi kipeo (apex bod) wa sekta binafsi, Mwamakimbullah (2016) alishauri uwepo wa sekretariati ya kitaifa itakayoundwa kiushindani na ambayo inawajibika kwa bodi kipeo. Mkutano Mkuu wa Mwaka utakuwa ndio chombo kikuu kabisa cha bodi kipeo hii.

Kielelezo na 1. Pendekezo la muundo wa sekta binafsi ya sekta ya misitu Tanzania

Figure 1. Proposed organization structure of the Tanzania private forestry sector



Ufunguo:

1-Chama cha wakulima wa miti Tanzania, 2- Wafanya biashara na wasafirishaji wa mazao ya misitu, 3- Mungano wa wapasua mbao, 4- Ushirika wa wenye viwanda vya mbao Tanzania, 5- Ushirika wa watia dawa mazao ya misitu, 6- Ushirika wa watengenezaji wa milango ya mbao Tanzania, 7- Ushirika wa makaontrakta wa ujenzi, 8- Ushirika wa wafanya biashara na wachomaji wa mkaa, 9- Ushirika wa mtandao wa mashirika na asasi zisizo za kiserikaliTanzania 10- Ushirika wa wamiliki wa misitu ya jamii.

Mapendekezo

Wadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika sera mpya:

- Serikali iwezeshe uanzishwaji wa chama chenye nguvu cha sekta ya misitu kikiwa na sura za uwakilishi maalumu wa mazao, biashara na minyororo ya thamani tofauti ya misitu.
- Serikali itaunda b**araza la ushauri na uratibu wa sekta ya misitu**, ambalo litaitisha angalau mikutano miwili kwa mwaka kuzungumzia shughuli za sekta ya misitu.
- Vyama vya wenye viwanda vitawakilishwa na vyombo mbalmbali vyenye shughuli zenye uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya misitu k.m. LMDA, Tanzania Forest Fund, na Kamati ya kumshauri Waziri (Ministerial Advisory Committee).
- Serikali itahakikisha kuwa utawala bora unashamiri katik sekta ya misitu kwa uwepo wa haki na uwazi katika shughuli zozote zitakazofanyika.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Uganda, Nigeria Afrika ya Kusini ni mifano ya kuigwa ya namna ambavyo serikali inaweza kushirikiana na sekta binafsi (kisanduku cha 3,4 na 5).

Sanduku 18: Baraza la ushauri na uratibu wa sera ya taifa ya misitu ya **Uganda** Nchini Uganda sera inatoa fursa ya kuwa na baraza linaloratibu na kupanga shughuli za sekta ya misitu. Baraza hilo hujumuisha kwa pamoja wawakilishi kutoka serikali, wizara zinazohusika na sekta ya misitu, serikali za mitaa, sekta binafsi na asasi za kijamii. Mfumo huo huhakikisha kuwa shughuli za sekta ya misitu zinaratibiwa na kusimamiwa ipasavyo kwa namana ambavyo shughuli za serikalikali kisekta zinaanishwa vizuri na majukumu yake hupunguzwa, ili baadhi yatekelezwe na sekta binafsi au asasi za kiraia zaidi.

Mfumo huo wa ushirikishwaji, huungwa mkono na chombo cha watalaam kitachonzishwa kwa kutokana na uwezo kifedha wa washikadau. Aina ya wafanya kazi na kazi itakazofanya yataendana na mahitaji yanayobadilika ya uratibu wa sekta. Isitoshe sera huwezesha baraza la ushauri kuwashirikisha wananchi, wadau wa kimataifa na yeyote mwenye nia njema kushiriki katika mijadala ya mara kwa mara ihusuyo sekta ya misitu, kwa nia ya kuiboresha na kutoa mchango kwenye vipau mbele vya kitaifa. Sera pia inao" mkakati *wa kuimarisha usimamizi wa sekta binafsi na kurahisiha mawasiliano, upatikanaji wa taarifa za masoko, na ushirikiano na maarifa yanayohitajika katika shughuli nzima za kupanda miti kibiashara"*

Sanduku la 19: Baraza la ushauri na uratibu wa sera ya taifa ya misitu ya **Nigeria**Nchini Nigeria, sera imeanzisha Kamati ya Kitaifa Kuendeleza ya Misitu, ambacho ndiyo chombo cha juu cha kutoa ishauri juu ya shughuli za misitu nchini. Wajumbe wa kamati hiyo ni Wakurugenzi wote wa serikali wanaohusika na misitu, wawakilishi wa baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali, wawakilishi wa sekta binafsi ya wapanda miti kibiashara, wakuu wa vitivo vya misistu wa vyuo vikuu, Mkurugenzi wa utafit wa misitu, na baadhi ya asasi zisizo za kiserikali. Mwenye kiti wa kamati ni mkurugenzi mkuu wa Misitu. Kamati hukutana mara mbili kwa mwaka kujadili utekelezaji wa Baraza la ushauri na uratibu wa sera ya taifa ya misitu ya **Nigeria**. Madhumuni ya baraza hili ni kuwezesha wananchi, washirika wa kimataifa na wadau wote waeze kutoa maoni yao kewnye majadiliano ya mara kwa mara yanayohusu sekta ya misitu ili kuboresha uratibu wa shughuli kisekta na kuzingatia vipaumbele vya kitaifa.

Sanduku la 20: Baraza la ushauri na uratibu wa sera ya taifa ya misitu ya Afrika **ya Kusini.** Huko Afrika Kusini, 'Forestry South Africa' huwakilisha wadau wote wa sekta ya misitu. Pia wanalo jukwaa la majadiliano, liitwalo the 'Commercial Forestry Liaison Forum' ambapo vyama vya misitu na serikali vinakutana kutengeneza mpango kazi wa mwaka. Baada yah apo, hukutana kila robo mwaka kujadili mafanikio na changamoto na kujenga mikakati ya pamoja ya kukabiliana na changamoto.

2.4.2 UTOAJI MOTISHA I NA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA AJILI YA UENDELEZAJI WA UPANDAJI MITI KIBIASHARA

Maoni ya wadau kwa mazingira ya Tanzania

Nchini Tanzania, Upandaji wa miti kibiashara hauna mpangilio mzuri na umekosa uongozi imara nyombo vya uendeshaji vyenye kuweza kufanya mabadilishano ya mawazo na uwakilishi kisekta. Sekta binafsi ya misitu bado ni change. Uendelezji wa sekta ya misitu Tanzania imetawaliwa na utegemezi wa misaada kutoka nchi za njen na njia za kujikwamua katika hali hiyo hazijazaa matunda. Mbinu za kifedha zilizopo kwa sasa hazijaweza kupata ufumbuzi wa tatizo hilo (Ngaga, 2011). Namna ya kupata fedha ni pamoja na kupata mikopo nafuu ya mabenki, nafuu za kodi, na malipo ya kupunguza hewa ukaa. Unafuu wa kodi umeziwezesha nchi nyingine kuendeleza upandaji miti wa kibiashara na kuifanya sekta hiyo kuwa muajiri mkubwa na kusababisha ongezeko kubwa na mazao ya misitu kwa matumizi ya ndani naya kuuza nchi za nje. Mataifa yanye mashamab makubwa ya miti yamekuwa yakitoa motisha ya unafuu kwa wawekezaji katika mashamba makubwa ya miti. Hali hiyo imefanyika vizuri katika nchi za Uruguay, Brazil, Nchi za Asia-Pacific, Costa Rica, Guatemala, Chile na nyinginezo. Kwa mfano endapo kodi ya mapato au VAT itapunguzwa kufikia kiwango kinachokubalika kwa pande zote (wadau na serikali) kunaweza kuinua kwa kasi upandaji miti kibiashara hapa nchini (PFP 2014). Mfumo wa ulipaji kodi unatakiwa uendane na namna kipindi cha usitawishaji wa miti hadi kuvunwa kilivyo kirefu, ili kuepuka utozaji kodi usiostahili.

Ukuzaji wa miti huchukua miaka mingi wakati mwingine hadi kufikia miaka 20. Wakulima huhitaji fedha kwa ajili ya uendeshaji na ustawishaji wa miti. Vile vile wanahitajji fedha kukidhi mahitaji ya familia zao wakati wakisubiti miti kukomaa. Ni jambo lisilosetirika kwa wakulima wamekuwa wakivuna miti michanga kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji yao ya msingi. Kwa namna nyingine ifahamike kuwa uboreshaji wa tekinolojia viwandani kwa lengo la kuinua uzalishaji na ufanisi, kunahitaji fedha za kuagiza mitambo na vifaa vipya. Wafanya biashara wadogo na wa kati , ingawaje wamekuwa wakifanya biashara za mazao ya misitu kwa kipindi kirefu , hata hivyo wameshindwa kukusanya mtaji wa kwawezesha kuagiza mashine na vifaa vipya.

Kwa kuwa mabenki na SACCOs hutoza riba za juu sana, pia imeshindikana kwa wao kukopa huko. Mara nyingine taasisi hizo za fedha hutoza riba hadi kufikia 20% ya feha iliyokopwa, na inatakiwa kurudishwa katika kipindi kifupi sana. Uwekaji wa dhamana ni njia mojawapo ya kupata mikopo, lakini hali hiyo imekuwa ngumu kwa kuwa dhamana ya mwakulima ni ardhi ambayo mara nyinene inakuwa haijapimwa na haina hati miliki. Utaratibu wa kupata hati una urasimu mrefu na ni ghali. Na isitoshe bei za upimaji ardhi na za kununua ardhi zimekuwa zikipanda kila mwaka, na kwa hakika ni za juu mno. Mabenki yamekuwa yakisuasua kukubali hatimiliki za kimila. Kwa hali hiyo, wadau wangependa kuona wakulima na wenye viwanda wanaandaliwa utaratibu wa kuwawezesha kupata fedha za kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia vipindi virefu vinavyotakiwa kustawisha miti na umuhimu wa kupata fedha kidogo kidogo hadi kufikia uvunaji.

Endapo serikali itatoa motisha ya mikopo huku ikitambua umuhimu wa faida zinazoonekana na zisizoonekana za mashamba makubwa ya miti pamoja na kuinua uchumi, kuna uhakika wa sekta ya panda miti kibiashara kupanuka.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika mswaada- jaribio wa sera ya Taifa ya Misitu:

● Serikali itaandaa mazingira mazuri na imara ya uwekezaji kwa wapanda miti kibiashara kwa njia ya kuwamotisha kuanzisha ushiriki wa wadau na serikali katiaka uzalishaji, uchakataji, uongezaji wa thamani ya bidhaa, uuzaji wa mazao ya misitu.

● Serikali itawezesha upatikanaji wa ruzuku na vivutio vinginevyo vya kifedha katika kuimarisha sekta ya panda miti kibiashara kama njia mojawapo ya kutambua umuhimu wa sekta hiyo katika kuinua uchumi kitaifa.

● TaFF (mfuko wa taifa wa misitu) itapanuliwa ili kukidhi mahitaji ya sekta ndogo ya upandaji miti kibiashara. La sivyo, badala yake utaanzishwa mfuko wa kuendeleza mashamba ya miti na viwanda vya misitu kwa ajili ya sekta binafsi.

● Serikali itaanzisha dawati maalum katika benki ya maendeleo endelevu na uwekezaji itakayokuwa na jukumu la kutoa mikopo kwa ajili ya uanzishwaji wa mashamba ya miti na viwanda vya misitu kwa ajili ya sekta binafsi. Huduma hiyo itazingatia mahitaji maalum yakiwemo kipindi kirefu ambacho huhitajika kabla ya miti kukomaa na kuvunwa.

● Serikali itatoa ruzuku kwa mashine zote zitakazoagizwa kwa ajili ya kuchakata mazao ya misitu, uongezaji wa thamani ya mazao, na uzalishaji wa bidhaa nyinginezo zitokanazo na mabaki ya mbao.

● Serikali itarahisisha utaratibu wa kupata hati miliki za ardhi kwa kupunguza gharama kupima ardhi na gharama nyingine husika kuwawezesha wamiliki kupata hati miliki za ardhi. Hati miliki za kimila zitatambuliwa kwa dhamana ya kujipatia mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na serikali itajitahidi kusawazisha jambo hili na sekta ya mabenki nchini.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku la 21: Tamko la Sera ya Taifa la **Nigeria** (2006*):*" Serikali itaimarisha utoaji wa ruzuku kwa viwanda vidogo vya misitu na uchakataji wa mazao ya misitu kwa kutambua vikwazo vya uwekezaji vinavyozikabili sekta binafsi."

Sanduku la 22: Tamko la Sera ya Taifa la **Zambia**

"*Kuandaa mazingira mazuri yasiyotetereka ya kuendeleza viwanda kwa kutoa motisha ya kuanzisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uzalishaji, ongezeko la thamani, uuzaji wa mazao ya misitu na utoaji huduma kwa kushirikiana na mamlaka husika".*

Sanduku la 23: Tamko la Sera ya Taifa la **Uganda** " Kukuza na kusaidia utoaji wa mitaji kifedha, kwa mfano Mfuko wa kuendeleza Misitu, na motisha za hali na mali katika kusukuma mbele juhudi za uwekezaji na kuhakikisha uwepo wa ruzuku za uendeshaji na uwekezaji."

2.4.3 MIUNDO MBINU YA VIJIJINI

Maoni ya wadau kwa mazingira ya Tanzania

Maeneo mengi amabapo kuna tekelezwa kilimo cha kupanda miti kibiashara, barabara zake hazipitiki wakati wote kwa urahisi. Kwa ujumla ni mbaya. Uchunguzi uliofanyika na Taasisi ya Uendelezaji wa Misitu Tanzania (FDT) iligundulika kuwa mbao zinazotoka katika mashamba yenye barabara mbovu huuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na mbao zinazotoka kwenye maeneo yenye barabara nzuri. Inatarajiwa kuwa mbao na magogo yatakayopelekwa viwandani siku za baadaye yatakuwa yanatoka Zaidi kwenye mashamba ya panda miti kibiashara. Hivyo ni muhimu miundo mbinu ya barabara ikawekwa sawa ili kukidhi mahitaji ya siku za usoni.Kwa kutaja mifano michache, maeneo hayo ni Rungwe, Kilolo, Mufindi, Njombe, na Ileje.Barabara hizo zitayafanya maeneo hayo yaweze kufikika kwa urahisi na kurahisisha uvunaji wa magogo toka maeneo hayo.Vilevile katika misitu ya hifadhi barabara ni mbovu na hazipitiki kipindi cha mvua.Uvunaji wa magogo na usafirishaji kutoka kwenye misitu ya serikali huwa wa gharama kubwa kutokana na uharibifu wa magari yaendayo misituni.Ukarabati na utengenezaji wa barabaa mpya ufanyike kwa kutumia fungu la linalotokana na mfuko wa LMDA. Usimamaizi wa mfuko wa LMDA uko chini ya TFS bila ya wadau wenye viwanda vya misitu kuchangia lolote katika mfuko huo. Inavyoonekana, kipao mbele cha matumizi ya mfuko huo kimekuwa tofauti na wadau wenye viwanda walivyotegemea.

Viwanda vimekuwa katika hali ya kupata umeme hafifu na usiotosheleza mahitaji. Umeme wa kutosha unahitajika kuvifanya viwanda kufanya kazi kwa uwezo wake na hivyo kuzalisha mazao yaliyo bora na yenye ushindani sokoni. Umeme utavifanya vijiendeshe kwa faida. Upatikanaji wa umeme vijijini kutawezesha uwekezaji zaidi wa viwanda vya kuchakata mazao ya misitu kuanzishwa huko huko ambako malighafi inakopatikana. Hali hiyo itainua uchumi wa sekta hiyo ya viwanda vya misitu.

Uimarishaji na ukarabati upya wa reli ya TAZARA ni muhimu sana kwa ufanisi wa viwanda vya misitu. Maana ni rahisi kusafirisha bidhaa kwa njia ya reli badala ya magari. Utumiaji wa reli hauna vikwazo vingi ikilinganishwa na usafirishaji kwa kutumia magari ya mizigo. Uimarishaji wa TAZARA utaiwezesha sekta ya viwanda kusafrisha bidhaa zake hadi Dar es Salaam penye soko kubwa kwa urahisi na kwa bei nafuu. Bidhaa hizo ni mbao, nguzo, na bidhaa nginginezo. Tukiwa na reli inayofanya kazi kwa ufanisi mkubwa kutaiwezesha sekta ya viwanda kuuza mazao yake nje ya nchi kwa urahisi kupitia bandari ya Da es Slaam. Mawazo ya aina hiyo ya kuimarisha reli ya TAZARA kwa nia ya kupunguza gharama za usafirishaji na bei za mazao ya misitu sokoni, yaliwahi kutolewa pia na PFP mwaka 2016. Kwa bahati mbaya TAZARA inajiendesha chini ya kiwango kilichotegemewa kutokan na usimamizi dhaifu na ukosefu wa fedha za kuliendesha shirika hilo, mambo ambayo sharti yatafutiwe ufumbuzi wa haraka.

Shughuli za uendeshaji bandarini zinatakiwa kufanyiwa mabadliko, kuliwezesha shirika la bandari kusafrisha mbao na mazao mengine ya misitu kwa ufanisi zaidi. Siku za nyuma haikuwa ajabu kwa meli kuondoka bandarini bila kupakia mizigo yoyote kutokana na urasimu uliosababisha ucheleweshaji wa meli hizo bandarini. Matokeo yake yamekuwa ni ya kuliingizia Taifa hasara kubwa ili kufidia gharama za meli hizo kuondoka na mizigo mfu/ bila kitu.

Mapendekezo

Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika mswaada- jaribio wa sera ya Taifa ya Misitu:

- Serikali itaendelea kukarabati na kuboresha miundo mbinu ya barabara vjijini husan katika maeneo yenye tija kibiashara kwa mfano maeneo yenye mashamba makubwa ya miti.

● Shughuli za reli ya TAZARA zitaimarishwa kuanikisha viwanda vya misitu kusafirisha bidhaa zao hadi Dar es Salaam penye soko kubwa

● Umeme utasambazwa vijijini kote na hasa vijiji vinavyozunguka mashamba makubwa ya miti. Serikali itahakikisha wateja wake wanapata umeme wenye uhakika na wa kiwango cha juu wakati wote.

● Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahakikisha mitandao ya simu na intaneti inaendeshwa kwa ufanisi ili kurahisiha maendeleo ya shughuli za biashara kufanyika

● Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahakikisha bandari zote zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa kurahisisha usafirishaji nje wa mazao ya misitu na uagizaji wa vifaa vya viwandani.

2.4.4 KUIMARISHA UTAFITI

Maoni ya wadau na mazingira ya Tanzania

Hivi sasa taasisi za utafiti zinaendeshwa chini ya uwezo wake kwa kutopewa fedha za kutosheleza mahitaji. TAFORI na TTSA wanashindwa kutoa huduma inavyopaswa kutokana na upungufu wa fedha na utalaam. Na huu ndio wakati muafaka wa kufanya utafiti ili kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya misitu. Nchi iko katika harakati ya kuongeza uzalishaji kutoka kwenye mashamba ya miti ili kukidhi mahitaji ya mazao ya misitu. Na wakati huo huo wakulima wanashindwa kupata mbegu bora za miti za kutosheleza mahitaji yao. Mfumuko wa magonjwa na wadudu waharibifu umekuwa ukiongezeka, lakini uwezo wa kufuatilia na kufahamu ukubwa wa tatizo hilo umekuwa mdogo. Madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi juu ya ukuzaji wa misitu hayajafahamika vema kwa wakulima wa miti. Wakulima wamebakia kutegemea kudra ya mwenyezi Mungu kuondokana na ukame na matokeo ya moto ambayo yamekuwa yakijirudia kwa muda mrefu.

Viwanda vya misitu vimejikita zaidi katika upasuaji wa mbao kana kwamba ndio shughuli pekee inayohitajika kufanyika. Utafiti unahitajika kufanyika kuviwezesha viwanda kuzalisha bidhaa mpya kuvifanya kupata faida kubwa zaidi. Majibu ya maswala haya yatapatikana kwa kuwekeza zaidi katika utafiti. Wadau wamekuwa wakiguswa mno na agenda ya sasa ya utafiti wa misitu kama kweli inakidhi mahitaji ya kitaifa. Wadau wanapenda kushirikishwa katika dhima nzima ya program za utafiti na kuona kuwa zinazingatia changamoto zilizopo sekta ya misitu. Changa moto nyingine inayowagusa sana wadau ni kuona kuwa taasisi za utafiti zimeshindwa kuwasilisha vilivyo matokeo ya ufafiti wao ambao wadau wanaweza kuyatumia matokeo hayo kutatua changamoto wanazokumbana nazo.

Mapendekezo

● Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya Taifa ya Misitu

● Serikali itaziongezea ruzuku taasisi zake za utafiti kuziongezea uwezo wa kufanya utafiti wa shughuli za misitu ipasavyo

● Utafiti utafanyika kwa kuzingatia mahitaji / vipau mbele halisi na wadau watashirikishwa katika kuandaa agenda za utafiti

●Sekta binafsi itahamasishwa kuchangia gharama za utafiti wa misitu kwa kutoa ruzuku, au kupitia

vyombo vingine vya fedha, pamoja na kuingia mikataba na taasisi za utafiti kufanya uchunguzi katika nyanja mbalmbali

● Serikali itaimarisha utafiti shirikishi kwa mapana zaidi, kwa mfano kushirikisha mashirika ya serikali, sekta binafsi, taasisi za kitaifa na kimataifa.

● Nyenzo za utafiti wa mazao ya misitu zitaanzishwa kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji wa aina nyingi za mazao ya misitu yaliyoongezewa thamani yatakayofikia soko.

Uzoefu kutoka nchi nyingine

Sanduku la 24: **South Africa** – Ushirikiano wa CSIR na wadau wengineJukumu la Shirika la CSIR la Afrika ya Kusini ni kuongeza ushirikiano wa karibu na vyombo mbalimbali vya serikali na sekta binafsi. CSIR wanaamini kuwa ni kwa njia ya kushirikiana ki- utafiti kutawezesha upatikanaji wa matukio chanya na ugunduzi wa mambo mbalimbali. Matatizo magumu yanahitaji ushirikiano katika kuyatatua. Ushirikiano hupanua uwezo wa kupambana na changamoto zinazojitokeza. CSIR hutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na mashirika, makampuni, taasisi za elimu, idara za serikali, na vyombo vinavyomilikiwa na serikali, na katika nyana zote za afya, nishati, viwanda, ulinzi na usalama na katika mambo ya kidijitali. CSIR hutoa mchango mkubwa kwa Afrika kufikia dhima yake ya kuwa bara lenye neema na amani, pia huchangia pakubwa katika ugunduzi mbalimbali kuiwezesha Afrika kupambana na changamoto za watu wake kwa kushirikiana na wadau waliobobea katika sayansi, uhandisi na teknologia.

2.4.5 ELIMU NA MAFUNZO

Maoni ya wadau na mazingira ya Tanzania

Upo upungufu mkubwa wa mabingwa na watalaam wenye uzoefu wa kuendesha na kusimamia ustawishaji wa miti kibiashara. Hali hii imetokana na hali halisi kuwa dhana ya upandaji miti kibiashara haifundishwi katika vyuo vikuu na vyuo vya kati vya misitu. Kwa kuzingatia faida zinazopatikana kiuchumi kutokana na kupanda miti kibiashara, inapendekezwa somo linalojitegemea la panda miti kibiashara liingizwe katika mitaala ya vyuo vikuu na vyuo vya kati. Mazoezi yawe ni sehemu kuu ya somo hilo.

Inaeleweka bayana kuwa serikali hutoa ruzuku ndogo isiyokidhi mahitaji ya vyuo vikuu na vuyo vya kati nchini. Matokeo ya upungufu wa ruzuku kumesababisha wanafunzi kutoka vyuoni bila kuiva vizuri kwa kutopata mazoezi ya kutosha kwenye mashamba makubwa ya miti. Tatizo la upungufu wa ruzuku ya serikali lipo pia kwa shughuli za utafiti. Wadau pia wamelalamikia upungufu mkubwa uliopo wa maseremala na mafundi mchundo kwa ajili ya kuendesha viwanda vya misitu. Tatizo hilo linahitaji ufumbuzi wa haraka kwa kutoa mafunzo ya ufundi wa viwanda vya misitu kwa kutumia Vyuo vya Ufundi Stadi, na kuwapa mazoezi ya kutosha viwandani, wanafunzi wanapokuwa vyuoni.

Waajiri wamekuwa hawajali kuwapa mafunzo wasimamizi na wafanyakazi kwa kipindi mrefu. Mafunzo yanayopendekezwa yangekuwa yenye manufaa sana kwa kuongeza uzalishaji, kupunguza gharama kuhakikisha usalama kazini. Vyuo vya ufundi Stadi kwa kushirikiana na wadau wangeweza kuandaa mafunzo kazini ya mara kwa mara kwa wafanyakazi. Wafanyakazi watakaofuzu mafunzo hayo watuzwe vyeti vya kufuzu mafunzo hayo. Hali hiyo itainua hamasa ya kufanya kazi na vipaji vyao kutambulika.

Mapendekezo

● Washikadau wanashauri vifungu vifuatavyo viingizwe katika rasimu ya sera ya Taifa ya Misitu

● Vyuo vikuu na vyuo vya kati vitapanga na kutekeleza mafunzo kwa vitendo yanayohusiana na upandaji miti kibiashara kwa madhumuni ya kupata wafanyakazi bora wa kusimamia na kuendesha sekta hiyo inayokua kwa kasi.

● Serikali itaongeza ruzuku kwa vyuo vikuu na vya kati kwa nia ya kuboresha mafunzo yanayotolewa na kuviwezesha vyuo hivyo kufanya utafiti kadri inavyostahili.

● Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau watashirikiana na mamlaka husika kuanzisha mafunzo kwa mafundi mchundo, mafundi wa kuunganisha sehemu za mashine, mafundi sanifu, mabwana miti na mabibi miti.

● Vyuo vikuu na vyuo vingine vya misitu vitaingiza mafunzo ya panda miti kibiashara kama somo mojawapo katika mitala yao ya mafunzo.

● Serikali itapanga mafunzo ya ufundi na kuwafumbua macho wafanya biashara wa wadogo na wa kati na kuwawezesha kuelewa teknologia stahiki.

MACHAPISHO YA REJEA

FBD. (2017). Forest Plantation and Woodlot Technical Guidelines. Forestry and Beekeeping Division, Ministry of Natural Resources and Tourism, Dar es Salaam, Tanzania.

FBD. (2017). Review of the National Forest Policy of 1998: The Status and the Way forward. Report by Forestry and Beekeeping Division dated 23 June 2017.

FDT. (2015). Baseline Tree Grower Survey Report. Forestry Development Trust, Iringa, Tanzania.

FDT. (2016). Mapping of forest plantation resources in Southern Highlands. Forestry Development Trust, Iringa, Tanzania.

Indufor. (2011). Timber Market Dynamics in Tanzania and in Key Export Markets. Indufor Oy, Finland.

Mwamakimbullah, R. (2016). Development of Private Forestry in Tanzania. African Forest Forum.

Ngaga, Y.M. (2011). Forest Plantations and Woodlots in Tanzania. Working Paper Series Volume 1. African Forest Forum, Nairobi, Kenya.

PFP. (2016). Value chain analysis of the plantation wood from Southern Highlands. Private Forestry Program, Iringa, Tanzania.

Unique. (2017). Tanzanian Wood Product Market Study. Report for the Forestry Development Trust. Unique Forestry and Land Use, Germany.

Forest policies from other countries

Federal Ministry of Environment Abuja (2006). National Forest Policy. Abuja Nigeria. 92pp

Government of Zimbabwe (Draft 2016). National Forest Policy. Harare, Zimbabwe. 31pp

Ministry of Lands and Natural Resources (2012). Ghana Forest and Wildlife Policy. Accra, Ghana. 24pp

Ministry of Lands, Natural Resouces and Environmental Protection (2014). National Forestry Policy. Lusaka Zambia. 23pp

Ministry of Water Affairs and Forestry, Sustainable Forest Development in South Africa. The Policy of the Government of National Unity. Pretoria, South Africa. 35pp

Ministry of Water, Lands and Environment. The Uganda Forestry Policy. Kampala Uganda. 36pp

URT. (1998). National Forest Policy, United Republic of Tanzania Printers, Dar es Salaam. 59pp

URT. (2016). National Forest Policy (draft October 2016). United Republic of Tanzania Printers, Dar es Salaam. 59pp

URT. (2002). National Forest Act No.14. United Republic of Tanzania Printers, Dar es Salaam. 1281pp
URT. (2004). Forest Regulations. United Republic of Tanzania Printers, Dar es Salaam. 119pp

Kiambatisho Na.1. Maoni ya washiriki ambao ni wadau binafsi wa panda miti kibiashara

Ili kuboresha ukusanyaji wa maoni na ushiriki wa wadau wa panda miti kibiashara kwenye mchakato wa kupitia sera ya misitu ulioanzishwa na serikali, Shirika la Uendelezaji Misitu Tanzania (FDT) lilitumia wataalamu wakuu washauri wa misitu wawili kuwezesha mchakato na kuratibu maoni ya wadau.

Wadau muhimu waligawanywa kwa makundi kuzingatia wanakotoka na ukubwa wa shughuli zao:

1. Wachakataji magogo
    - *Wafanya biashara wa kati wa kuchakata magogo;* ambao ni pamoja na wapasua mbao wenye mashine za kuhamisha na wenye misumeno mikubwa ya kusimama n.k
    - *Wafanya biashara wa kati wa kuchakata magogo:* viwanda vya mbao, watengenezaji wa vinia, viwanda vya samani, viwanda vinavyotengeneza bidhaa za mazao ya miti yaliyoongezwa thamani, pamoja na vyama vya ushirika kama UWAMBA, SAFIA, NOFIA na SHIVIMITA.
    - *Wafavya biashara wa nguzo:* Waandaaji na wauzaji wa nguzo zilizotiwa dawa.
2. Makampuni ya misitu
    - *Makampuni yenye mashamba makubwa na viwanda:* Sao Hill Industries, Mufindi Paper Mill, TANWAT, New Forest Company na KVTC, pamoja na Tanzania Chamber of Commerce na vilevile mashirika yaliyowakilisha viwanda hivyo k.m. African Forestry.
3. Wamiliki wa mashamba ya miti
    - *Vyama vya wakulima wa miti:* Wajumbe wawili kila wilaya na kiongozi wa shirikisho la vyama.
    - *Wakulima wa miti wa kati:* mchanganyiko wa wawekezaji na wakulima wa miti waishio mijini na vijijini: wakijumuisha mshirika ya makanisa, walimaji wa chai na walimaji wa tumbaku.
4. Watoaji wa huduma kwa wakulima wa mashamba ya miti
    - *Watoa huduma kwa wakulima:* Waendeshaji vitalu vya miche ya miti, makandarasi wa mashamba makubwa ya miti na wasambazaji wa miche.
    - *Wafanya biashara wa mbao na nguzo na wasafirishaji pamoja na wauzaji wa nguzo.*

Isitoshe, shughuli za misitu na sera za misitu za nchi nyingine za Kiafrika zilichambuliwa ili kutambua zinazofaa kuingizwa kwenye sera mpya ya misitu.

Warsha kadhaa za kuchambua sera

Kila kundi lililohudhuria lilikuwa na warsha kadha zilizoandaliwa kwa siku moja mjini Njombe na Mafinga, ili kuwawezesha washiriki wenye viwanda vya kuchakata mazao ya misitu na wakulima kuhudhuria kwa wingi wao. Orodha ya waliohudhuria imeonyeshwa hapa chini:

Kongamano/ warsha ya usanisi na kuhalalisha / kuthibitisha sera ya misitu iliendeshwa Mafinga tarehe 18 Augosti kuwawezesha wadau kupitia maoni yahusuyo rasimu ya sera ya misitu yaliyotolewa na vikundi mbalimbali katika mikutano yao ya awali / iliyotangulia kujadili rasimu hiyo, na kuwasilishwa kwa Timu ya Kitaifa ya kupitia upya sera kwenye mkutano wa kanda ya nyanda za juu kusini. Mkutano uliokubali kushirikiana kwa hali ya juu katika shughuli nzima ya kupitia upya sera ya misitu.

Jedwali: Orodha ya wapanda miti kibiashara waliohudhuria warsha ya kuchambua/ kupitia upya sera mpya ya misitu (orodha ya mahudhurio na sahihi zao inapatikana)

Tarehe	Aina ya Mwana warsha	S	Jina	Kampuni/ Shirika	Atokako
19.06.2017	Mashirika madogo ya mbao	1	Oscar M. Kaduma	Mufindi by Products	Mafinga
		2	Nelson M. Betson	Edda Saw mill	
		3	Anyelwisye N. Mahenge	Mena Wood	
		4	Aziz E. Feer	Aziz E. Feer	
		5	Mariam S. Mbarouk	Marium Mbarouk	
		6	Fred N. Sentam	Sentam Timber	
		7	Jeniffer Kimario	Kimario Timber	
		8	Farida M. Haule	Farida Haule	
		9	Yona Mwakanjuki	Paulyona Timber	
		1	Mary Zablon Simba	Wambi Timber	
		1	William Mgowule	Manhattan Investment	
		1	Vitus Mponzi	Mufindi Wood Plantations	
		1	G. K Mosha	MUET	
20.06.2017	Mashirika ya kati ya mbao	1	Mussa Magelanga	TABEA	Mafinga
		2	Constantine Christine	KOMAS	
		3	Elfas Kaboda	Benon Saw Mill	
		4	Halid Sheketo	Halid Entreprise	
		5	Castory Sanga	Green Timber	
		6	Leonard Mahenda	Qwihaya General Traders	
		7	Seleman Mwenda	CF Saw Mill	
		8	Beruto K. Baruma	BEKAN Company	
		9	Damas C. Ng'umbi	DARODESHEDEA	
		1	Henry Lukambinga	Ihembe Timber	
21.06.2017	Wenye mashamba ya kati ya tumbaku na chai	1	Owden Mwaikema	WATCO	Mafinga
		2	Fr. Arnold Ngolle	KILOCHA TEA FARM	

Tarehe	Aina ya Mwana warsha	Sn	Jina	Kampuni/ Shirika	Atokako
		3	Rick Ghaui	JILANJO LM	
		4	Mr. Matekeleza	Matekeleza and	
		5	Method Changa	Method Changa	
		6	Kasian Chang'a	MTC	
		7	Joseph R. Ng'umbi	Joseph Ng'umbi	
		8	Cheddy Ng'umbi	Cheddy Ng'umbi	
		9	Hawad Rashid	Hawad Rashid	
		1	Daniel Msigwa	Msigwa Logistics	
		2	Julius S. Sangija	SHEDA General	
23.06.2017	Wahifadhi wa magogo na nguzo kwa dawa	3	Leonard Mahenda	Qwihaya General	Mafinga
		4	Abdallah	Uyole Investment	
		5	John Mwauri	Sao Hill Industries	
		1	Lionel Dlamini	New Forests	
04.07.2017	Makampuni makubwa ya mashamba ya miti	2	Victor Kimey	Green Resources	Mafinga
		3	Antery Kiwale	TANWAT	
		1	Yohana S.	TGA	
		2	Junus K. Mhanje	TGA	
		3	Kastory M. Timbula	PFP	
		4	Laban S. Mgimba	TGA	
		5	Lukas N. Payovela	TGA	
05.07.2017	Wakulima wadogo wa mashamba ya miti na wasambazaji wa mbegu za miti	6	Ezekiel Sanga	TGA	Njombe
		7	Juhani Pekkala	PFP	
		8	Steven Sallu	Jambe Agro	
		9	Venance W.	TGA	
		10	Jerda E. Kikoti	TGA	
		11	Adriano E.	TGA	
		12	Lucy O. Ngailo	TGA	

Tarehe	Aina ya Mwana warsha	Sn	Jina	Kampuni/ Shirika	Atokako
		13	Dominicius A. Mganwa	TGA	
		14	Lazarus Mbillinyi	TGA	
		15	Peter Mbengwa	TGA	
		16	Happy Nyato	TGA	
		17	Filoteus Lwekela	TGA	
		18	Raymond O. Haule	TGA	
18.08.2017	Warsha ya kuhalalisha na kusanisi sera ya misitu	1	Willy Mgowole	Halidi Enterprise	Mafinga
		2	Owden Mwaikela	Wakulima Tea	
		3	Rick Ghaui	Jilanjo	
		4	Matekelza Chang'a	Matekelza	
		5	Kasian Chang'a	Mufindi Tea	
		6	Yohana Kikungwe	TGA	
		7	Kastory Timbula	TGA	
		8	Laban Mgimba	TGA	
		9	Lazarus Mbilinyi	TGA	
		10	Jerida Kikoti	TGA	
		11	Happy Nyato	TGA	
		12	Lucas Payovela	TGA	
		13	Lucy Ngailo	TGA	
		14	Ben Sulus	SHIVIMITA	
		15	Alphonce Kipande	Manhattan Enterprises	